

**KLOP AULA RED BULL**

UKURASA 21

**IDADI** ya watu nchini yafikia milioni 65

UKURASA 3

**THRDC** yakabidhi vyama vya siasa ilani ya uchaguzi

UKURASA 3



**GACHAGUA** mambo magumu Kenya, seneti yashikilia hatima yake

UKURASA 19


# Nipashe

Alhamisi Oktoba 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0581825

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital


# CCM yapinga vikali hoja ya CHADEMA

## KATIBU Mkuu Nchimbi amjia juu Katibu Mkuu Mnyika...*Ukurasa wa 2*



## KCB yapanda miti mikoa minane kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja

**Na Mwandishi Wetu**

KCB Bank inaongoza juhudi za maendeleo endelevu kama kampuni inayowajibika kwa jamii kwa kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) - Lengo Na. 14 kupitia mkakati madhubuti unaojikita katika nguzo za kiuchumi, kijamii na mazingira.

Katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, KCB Bank, ikiwakilishwa na Paschal Machango kwa niaba ya Cosmas Kimario, Mkurugenzi wa Biashara wa Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji - KCB Bank Tanzania, imechukua hatua muhimu ya kimazingira kwa kupanda miti zaidi ya 1,500 katika...

ENDELEA UKURASA WA 8



Paschal Machango akimwagilia mti uliopandwa katika Shule ya Msingi Mbagala Anex, Dar es Salaam jana, akimwakilisha Mkurugenzi wa Biashara wa Kanda wa KCB Group, Cosmas Kimario, pamoja Mkurugenzi Mtendaji - KCB Bank Tanzania. Benki hiyo imepanda miti zaidi ya 1,500 katika mikoa mbalimbali ya uendeshaji wake nchini. **PICHA: KCB**

UKURASA WA 24

## SIMBA, YANGA ZAFUNGUKA

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema malengo yake ni kumaliza kinara katika Kundi A kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika watani zao, Yanga...





## Wavuka mpaka kufadhili kilimo cha bangi nchini

UKURASA 2

# Kabudi aonya R4 za Rais Samia kutumika vibaya

UKURASA 2

**MICHEZO** STARS, DRC CONGO MAJARIBUNI UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Wavuka mpaka kufadhili kilimo cha bangi nchini

**Na Zanura Mollel**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema uchunguzi wake umebaini kilimo cha bangi mkoani Mara, unafadhiliwa na raia wa nchi jirani ambao huwapa mitaji wakulima wa Tarime ili kuwezesha kilimo hicho.

Imesema kuwa baada ya bangi kukomaa na kuwa tayari kwa mavuno, huvunwa na kusafirisha kwenda kuuzwa katika taifa hilo (jina limehifadhiwa).

Hayo yalibainishwa juzi na Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, Aretas Lyimo wakati wa utekeletezaji ekari 3007.3 za mashamba ya bangi na kukamata bangi kavu kilo 7832.5 katika wilaya ya Tarime na Serengeti.

"Tunatoa miezi mitatu kwa wananchi wa mkoa wa Mara kuhakikisha wanaachana kabisa na kilimo cha bangi. Baada ya muda huo, tutafanya operesheni kubwa kwa namna nyingine na kuhakikisha maeneo haya yanabadilishiwa matumizi," alisema Kamishna Lyimo.

Operesheni hiyo ya wiki tatu imefanyika katika vijiji vya Matongo, Nyarwana na Weigita vilivyoko bonde la Masinki, pia vijiji vya Nkerege, Kembwe, Nyakunguru na Iseresere pamoja na eneo la bonde la Mto Mara, watu 17 wakikamatwa.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Meja Edward Gowele, alithibitisha wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya kilimo cha bangi hususani katika eneo la bonde la Mto Mara na tayari serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti.

Ofisa wa Maji wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria Dakio la Mara, Mwita Mataro alisema, "Tumejionea hali halisi ya bonde na tumeshuhudia zao la bangi likiwa limelimwa katika bonde la Mto Mara. Sheria za rasilimali za maji haziruhusu kilimo haramu cha bangi.

"Hata mazao mengine halali yanapaswa kulimwa umbali wa mita 60 kutoka mtoni. Hao wanaolima bangi ni sehemu ya watu wanaoharibu vyanzo vya maji kwa sababu mwisho wa siku huu udongo wote mvua itakaponyesha tope lote linatiririkka kwenda kwenye mto."

Ofisa Kilimo - Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, Lepapa Molel alisema wakulima wengi wanalima bangi kwa kutegemea maji yanayotoka Mto Mara. "Nashauri wakulima wageuke na kuanza kulima mazao ya chakula yanayoweza kuwapa chakula na fedha kuliko bangi," alisema.

Mwenyekiti wa Mila Ukoo wa Wasweta, Mzee Julius Matiku, alisema, "Tumekubaliana kuteketeza bangi ili kuondoa tatizo hili la kukimbiakimbia. "Kijana atakayekamatwa akilima bangi, atatozwa faini ya ng'ombe watano, mzee wa mila analo jukumu la kuhakikisha sheria zinaheshimiwa katika kijiji."

Katibu wa Mila Burima, Marwa Nyawise alisema wameamua kuteketeza bangi ili walime mazao mengine kama mahindi, ufuta na kuendelea kufuga mifugo yao katika pori hilo.

# CCM yajibu hoja ya CHADEMA

**Na Halfani Chusi,** MASWA



Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi,

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimejibu hoja iliyotolewa juzi na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, kuwa ni dalili kwamba wapinzani wao hao kisiasa wameona watashindwa uchaguzi, hivyo wanatafuta visingizio.

Juzi, Mnyika alizungumza na vyombo vya habari na kueleza kuwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) haijafanya jitihada za kutosha kuelimisha wananchi kuhusiana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema ni muhimu wananchi wakajitokeza kujiandikisha kwenye Daftari la Wakazi kuanzia kesho hadi Oktoba 20 mwaka huu na wameamua kuongeza kasi kwa kuwa wameona suala hilo halijapewa uzito mkubwa wakati ziku za kujiandikisha zinakaribia.

Akijibu hoja hiyo jana, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akiwa ziarani eneo la Malampaka, wilayani Maswa, mkoani Simiyu, alisema hakuna ukweli wowote juu ya hoja za Katibu Mkuu Mnyika kwa kuwa kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika.

Alisema halmashauri zilipewa jukumu la kusimamia uandikishaji huo kwa mujibu wa mwongozo na kanuni za Serikali ya Mitaa.

"Nimeona katika mitandao ya kijamii kiongozi mmoja wa upinzani (bila kumtaja jina), analalamika kuhusu suala hilo kwamba CCM na TAMISEMI kwa makusudi hawahamasishi watu kujiandikisha, hawahamasishi watu kupiga kura. Nikacheka, nikasema 'hawa wenzetu hawa', sisi mikoa yote 18 tunazunguka tunahamasisha, si mnatusikia huko?

"Tunahamasisha watu wajiandikishe, watu wapige kura wanaCCM na wasio wanaCCM kwa sababu tunajua hata wasiokuwa wanaCCM wanaipigia kura CCM kwa sababu ya kazi nzuri ambayo chama chetu kimefanya," alisema.

Katibu Mkuu Nchimbi alisema alisikiliza na kutafakari kauli hiyo na anadhani tayari chama hicho kimeshajua hali ni mbaya; "hakitapata kitu katika uchaguzi huu, hivyo kinaanza kutafuta kisingizio mapema".

"Kama wanavyofanya zile timu kubwa... oooh walitangulia wakaruka ukuta, kwani ukuta ndiyo unaocheza? Watu ndiyo wanaocheza, visingizio waache, twendeni tukatafute kura, wao waombe na sisi tuombe, visingizio hivi ni vya kitoto," alisema Dk. Nchimbi huku akishangiliwa.

Katibu Mkuu huyo pia alipongeza uongozi wa CCM mkoani Simiyu kwa kuendelea kukiunganisha chama, akisisitiza kuwa amehamasika na namna alivyopokewa kwa hamasa kubwa.

"Si kila mwananke anaweza kuwa kiongozi, kama ilivyo kwa wanamume kwamba si kila mwanamume anaweza kuwa kiongozi.

Sasa hivi Afrika nzima inatamani kuwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Wengi walidhani hatoweza kuvaa viatu vya Dk. John Magufuli, lakini ameweza na anafanya mambo makubwa.

"Ninyi wenyewe mmeona namna anavyofanya kazi kwa vitendo, miradi mikubwa ya maendeleo inaonekana, shule, huduma za afya ya uzazi kwa kina mama," alisema.

Aliyekuwa Kada wa CHADEMA na kuhamia CCM, Peter Msigwa alisema kuwa kwa uzoefu wake ndani ya CHADEMA kwa miaka 20, amebaini hawana uwezo wa kuongoza nchi.

Katika ziara hiyo, Balozi Dk. Nchimbi ameambatana na Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla na Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (Suki), Rabia Hamid Abdalla.

Ziara hiyo pia imejikita katika kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 - 2025, kusikiliza kero na changamoto za wananchi kisha kuzitafutia majawabu na kuhamasisha uimara wa CCM kuanzia ngazi ya mashina.

# Kabudi aonya matumizi mabaya ya 4R kuingilia mamlaka, uamuzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, ameonya matumizi mabaya ya dhana ya 4R za Rais Samia Suluhu Hassan, kutumika kama kichaka cha watu kufanya mambo yanayovunja sheria za nchi, ikiwamo kuingilia mamlaka ya vyombo vya uamuzi.

Prof. Kabudi alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao cha Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema watu hawapaswi kutumia vibaya dhana hiyo ya Rais kwa kufanya mambo ambayo yanavunja sheria na kufikiri kuwa wanayo haki ya kufanya jambo ambalo linaweza kuingilia uhuru wa vyombo vya uamuzi.

"Dhana hii ya 4R isiwe kichaka cha watu kufanya mambo ya fujo na kuingilia mamlaka za vyombo vya uamuzi na kuvunja sheria za nchi bali itumike kwa misingi iliyokusudiwa bila kuhatarisha umoja wetu na kuzingatia hadhi ya kila mmoja wetu," alisema Prof. Kabudi.

Alisema taasisi hizo tatu zinapaswa kufanya mambo yao kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni bila ya kuathiriwa na mihemuko ya kundi au mtu fulani.

Pia alizitaka taasisi zote zilizopo katika masuala ya haki jinai nchini, kuimarisha weledi katika shughuli zote za upelelezi ili kumaliza tatizo la mrundikano wa mashauri na mahabusu gerezani.

Alisema moja kati ya changamoto zinazochangia ongezeko la mrundikano wa mashauri pamoja na mahabusu, ni kasi ndogo ya upelelezi, hivyo ipo haja taasisi zote zinazohusika na haki jinai kuongeza ufanisi kumaliza hali hiyo.

Vilevile, aliwataka kuweka utaratibu wa kukutana mara kwa mara ili kufahamiana na kila mmoja kujua majukumu yake yanaishia wapi na ya mwenzake yanaanzia wapi, ili kurahisisha uendeshaji wa mashauri na kutoa haki kwa wakati.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu mwakani, Prof. Kabudi, aliagiza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, TAKUKURU na Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai kusimamia sheria ili uchaguzi huo uwe huru na wa haki.

"Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa na mwakani 2025 ni uchaguzi mkuu niwaombe msimamie sheria za uchaguzi, ili nchi yetu kuendelea na utulivu na amani iliyopo na kuepuka mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza katika mataifa mengine," alisema.

Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania (DPP), Sylvester Mwakitalu, alisema kikao hicho kinachokutanisha ofisi zinazounda utatu katika masuala ya haki jinai nchini, lengo lake ni kujadili changamoto mbalimbali katika sekta hiyo pamoja na kuandaa mikakati ya kupata suluhu.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila, alisema tangu kuanzishwa kwa umoja wa taasisi hizo, kasi ya uendeshaji mashauri imeongezeka na kusaidia kupunguza mrundikano wa mahabusu katika magereza.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya miaka mitatu iliyopita kuhusu utolewaji wa haki jinai nchini, ilifichua udhaifu mkubwa katika eneo hilo.

Ndiyo chanzo cha Rais Samia kuunda tume ya kuishauri serikali hatua za kuchukua kuondoa dosari zilizoibuliwa na mdhibiti.

HABARI KITAIFA

# Idadi ya watu nchini sasa milioni 65

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

IDADI ya watu nchini imeongezeka na kufikia milioni 65 mwaka huu kutoka milioni 61.7 iliyotangazwa wakati wa kutoa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema hayo jana wakati wa kongamano la wanawake na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Singida linalofanyika mjini Singida kwa kuwa lina lengo la kuwahamasisha wanawake kushiriki uchaguzi huo unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

"Nchi yetu imebarikiwa sana, tulikuwa na Sensa ya Watu na Makazi 2022, sasa hivi nchi yetu ina watu milioni 65 kwa makadirio ya mwaka 2024 na kwa Mkoa wa Singida wamefikia watu milioni 2.1 kutoka watu 2,008,000 waliokuwapo mwaka 2022," alisema.

Dk. Chuwa alisema kuwa idadi ya wanawake inaendelea kuwa kubwa, hivyo wajitokeze kujiandikisha na kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda aliwataka wanawake kuhakikisha wanajiandikisha, wagombea nafasi za uongozi na kwenda kupiga kura wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu; wasipofanya hivyo "itakuwa imekula kwao, kwani ushindi ni hesabu".

Anne ambaye ni Kamisaa wa Sensa alisema wanawake wanatakiwa kufanya maajabu katika uchaguzi huo kwa kuhakikisha Rais anakuwa mwanamke, wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa nao wanakuwa wanawake "hadi dunia ishangae".

"Tujiandikishe na tukapige kura, tusipopiga kura imekula kwetu kwani ushindi ni hesabu, maana mama (Rais Samia) anasifika sana, mara asante kwa maji, asante kwa barabara! Basi ninyi mnafikiri mama anapita asubuhi? Hapana!

Ni hesabu, hata viongozi wetu wa mitaa, vitongoni ni hesabu," alisema.

Anne alisema wanawake wanapenda kudharau vitu vingi, lakini katika suala la uchaguzi wanawake wawapeleke watoto kujiandikisha na kupiga kura ili kupata viongozi wengi wanawake kwa kuwa uwekezaji katika nchi unataka demokrasia.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema wanawake kwa kutambua kuwa wao ndio nguzo ya uchumi, wahakikishe wanasimamia malezi ya watoto wao na wasiwaache walelewe na mitandao ya kijamii.

Halima alisema kuwa katika Mkoa wa Singida, zipo zaidi ya Sh. bilioni 2.1 benki ambazo zimetengwa na halmashauri kutoka fungu la asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya kuwakopesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema kongamano hilo ni kwa ajili ya kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Alisema uwakilishi wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi katika mkoa wa Singida ni mdogo. Kati ya vitongoji 2,000 vya mkoa huo, uwakilishi wa wanawake kwenye uongozi ni asilimia nne tu.

Dk. Mganga alisema kuwa katika vijiji 441 vya mkoa huo, ni wanawake watano tu waliopata nafasi ya uongozi kuwa wenyeviti wa vijiji sawa na asilimia moja tu wakati katika kata 136 ni kata nne tu ambazo wanawake wanaziwakilisha kwa kushinda uchaguzi wa udiwani.

"Katika Manispaa ya Singida kuna mitaa 53 lakini wanawake waliothubutu kuchukua fomu na kushinda ni watatu tu wakati katika nafasi ya ujumbe kati ya nafasi 11,000 za wajumbe wa serikali za mitaa, wanawake 3,125 ndio wajumbe wa serikali za mitaa," alisema.

Dk. Mganga alisema kuwa kutokana na uwakilishi mdogo wa wanawake katika uongozi, uongozi wa Mkoa wa Singida umeona hauwezi kunyamazia suala hili, hivyo umekuwa unaandaa makongamano ili kuwapa uelewa na ujasiri wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.



Meneja wa Kitengo cha Kukabiliana na maafa cha Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Samwel Katamba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Mikocheni Dar es Salaam jana, kuhusu uamuzi wa chama hicho, kupeleka wafanyakazi wa kujitolea maeneo ya mipakani kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa MPOX. Kulia ni ofisa wa kukabiliana na maafa, Christa Christian na Mtaalamu wa Saikolojia, Maudline Tarazo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Alama mchango wa Nyerere ukombozi bara la Afrika inaishi'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Balozi wa China nchini, Suo Peng, kesho atawasilisha andiko katika mdahalo wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere lenye kichwa cha habari 'Alama Isiyofutika ya Mchango wa Mwalimu Nyerere na Tanzania katika Ukombozi wa Bara la Afrika'.

Chama cha Kikomunisti cha Jamhuri ya Watu wa China (CPC) kinathamini uongozi na mchango wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha Mkoa wa Pwani jana, Mkuu wa Shule hiyo, Professa, Marcelina Chijoriga, alisema Naibu Balozi huyo wa China atawasilisha andiko hilo katika mdahalo wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere utakaofanyika katika shule hiyo, Kibaha kwa Mfipa.

"Historia iko wazi ni kwa namna gani ambavyo Tanzania iligeuka kuwa makao makuu ya vyama vya ukombozi vya Angola's Popular Movement for the Liberation of Angola(MPLA), National Front for the Liberation of Angola (FNLA) na kile kilichokuja kugeuka kuwa kikundi cha waasi cha National Union for the Total Independence of Angola (UNITA), vyote kutoka Angola na Zimbabwe vikiwa ni (ZANU PF) na (ZAPU PF)," alisema Professa Chijoriga kuwa yote hayo Mwalimu Nyerere aliyafanya kwa kujitolea na bila woga na kwa kuijua historia, Wachina kupitia Naibu Balozi wanataka kuiambia dunia kuwa mchango wa Mwalimu Nyerere bado unaishi, jina la Mwalimu Nyerere linaishi pia.

Kwa mujibu wa Professa Chijoriga, msaada wa Tanzania kwa wapigania uhuru ambao ulifikia hata Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) kwenda mstari wa mbele haukuishia kwa MPLA, FNLA au ZANU PF pekee bali ulihusisha pia vyama vya kupigania ukombozi vya Afrika Kusini kama African National Congress (ANC), Pan-Africanist Congress (PAC) South African Communist Party (SACP) pia FRELIMO ya Msumbiji.

Mdahalo huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wageni 200 kutoka Afrika Kusini, China, Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Ghana, Nchi za Nordic, Umoja wa Afrika (AU) na Nigeria, wazungumzaji wengine ni Stephen Wassira, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) na Kamati Kuu ya NEC, Mkuu wa Majeshi ya Zimbabwe, Zimbabwe Defence Forces (ZDF), Luteni Jenerali, Anselem Sanyatwe na mpiganaji katika Jeshi la kupigania Uhuru la Namibia lililojulikana kwa jina la Peoples' Liberation Army of Namibia (PLAN), Dk. Charles Mubita. Mdahalo huo utakaofunguliwa na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete utawaona pia Kanali mstaafu wa JWTZ, Joseph Simbakalia, akiwasilisha andiko lenye maudhui ya mchango mahsusi wa Mwalimu Nyerere katika mapambano ya ukombozi wa bara la Afrika.

# THRDC yakabidhi vyama vya siasa ilani ya uchaguzi

**Na Pilly Kigome**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umekikabidhi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ilani ya uchaguzi ya mwaka 2024/29 iliyopendekezwa na Azaki za Kiraia zipatazo 300 na kuweka kipaumbele kikuu Katiba mpya.

Akizungumza katika makao makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji THRDC, Onesmo Olengurumwa, alikiomba chama hicho kuweka nguvu kuipata Katiba mpya pamoja na mapendekezo yaliyoainishwa katika ilani hiyo.

Olengurumwa alisema kuelekea 'Tanzania Tuitakayo' Asaki hizo zimetoa vipaumbele vingi pamoja na ulinzi wa uwajibikaji wa rasilimali za nchi, kupambana na ufisadi na rushwa uliopo nchini, mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa waathirika wakubwa ni wakulima na wafugaji ambao asilimia kubwa ya wananchi wanategemea rasilimali hizo.

Kuhusu haki za binadamu, walitoa mapendekezo viongozi watakaochaguliwa katika ngazi zote, lazima wawe watetezi wa haki za binadamu, mgawanyo wa madaraka, kulinda Tunu za Kitaifa ambazo ni umoja, undugu, mshikamano, uwazi na uwajibikaji katika ushirikishwaji wa wananchi ikiwamo na kusimamia uadilifu.

Alisema viongozi wanaotafuta ridhaa ni lazima waheshimu michakato yote ya kidemokrasia, viongozi wawe tayari kulileta taifa pamoja, kukubali kukosolewa na kudumisha uvumilivu.

"Kupitia mapendekezo haya tunayowakabidhi vyama vya siasa kwa pamoja tukishirikiana tutafanikiwa kuipata Tanzania tuitakayo, lakini kipaumbele chetu namba moja kwa vyama hivi tuongeze nguvu tupate Katiba mpya," alisema Olengurumwa.

Naye Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema wamepokea kwa mikono miwili ilani hiyo kwa kuwa wamekuja kipindi mwafaka cha mchakato wa kukamilisha ilani yao ya uchaguzi na watapitia vyema ilani hiyo na kuahidi kuwa pamoja kwa kuwa wamefurahishwa na asasi hizo kuungana nao katika kuipigia kelele Katiba mpya.

Alisema Katiba mpya ndiyo itakayofanya kubadilika kwa mambo mengi ikiwamo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kuwa wananchi wengi hususani vijijini wanalia na ugumu wa maisha.

Aidha, aliziomba Azaki hizo kukaa upya na kuliangalia kwa kina suala la ukuaji wa deni la taifa pamoja na kusaidia kuhubiri kwa wananchi kuhusu suala la wananchi kujiandikisha katika daftari la wapigakura kwa kuwa wengi wanaonekana hawana elimu na wanaamini ukiwa na kitambulisho cha mpigakura inatosha kupiga kura.

Vilevile, alibainisha kuwa katika suala la uchaguzi huru nchini, Chadema kinasema sheria zilizotungwa kuhusu uchaguzi bado si rafiki na haziwezeshi kuwa na uchaguzi huru na haki nchini Tanzania.

Tayari THRDC imeshatembelea Chama cha NCCR Mageuzi, ACT-Wazalendo, CUF, CHAUMMA na ADC.

# HABARI PICHANI





Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank, Silvest Arumasi (kushoto), akimkabidhi cheti cha shukurani mmoja wa wateja wa benki hiyo, Twaib  Msechu, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika katika ofisi za tawi la Ubungo Plaza jana.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania (BOA), Esther Cecil Maruma (wa pili kushoto), akimkabidhi mteja zawadi, ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, hafla iliyofanyika katika ofisi za benki hiyo, Tawi la NDC.




Grace Fenta, Mwakilishi wa Huduma za Kiufundi za Uchimbaji kutoka Geita Gold Mining Limited (GGML), akimwelezea mgeni kuhusu mipango, ratiba, na muundo wa chini ya ardhi wakati wa Maonyesho ya 7 ya Uchimbaji na Teknolojia huko Geita. GGML imehusika kama mdhamini mkuu wa maonyesho hayo kwa mara ya saba mfululizo.



Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, akimsikiliza mteja ili kumhudumia.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Stanbic, Manzi Rwegasira (wa pili kulia), akikata keki pamoja na wateja ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Huduma kwa Wateja.



Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, akiwa na baadhi ya watumishi wa idara ya elimu kwa mlipakodi na mawasiliano waliofika katika ofisi za TRA Makao Makuu katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MUSSA AMEIR-TRA**

# Ripoti yaainisha vikwazo vikuu vitano elimu kwa mtoto wa kike

**Na Elizabeth Zaya**

RIPOTI mpya ya Shirika la Msichana Initiative inaonesha umaskini, ndoa za utotoni, mitazamo mibovu ya wazazi, kutojua kusoma na kuandika na kukosekana kwa mazingira rafiki na safi shuleni ndio vikwazo vikuu vinavyotishia upatikanaji elimu bora kwa watoto wa kike nchini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, wasichana kutoka maeneo mbalimbali nchini wanaendelea kukumbwa na vitendo vya ukiukwaji haki za msingi huku wengi wao wakikumbwa na ukatili wa kisaikolojia, ndoa za utotoni na upatikanaji mdogo wa elimu bora.

Ripoti hiyo iliyopewa jina la 'Uchambuzi wa Hali ya Haki na Ustawi wa Mtoto wa Kike', inabainisha kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali na wadau katika kuinua maendeleo ya mtoto wa kike, wengi wao bado wanashindwa kutimiza ndoto zao za msingi.

Miongoni mwa wasichana wanaokumbwa zaidi na vitendo hivyo vya ukatili ni wale wanaoishi vijijini na wenye ulemavu huku mila na desturi pamoja na mfumo dume vikitajwa kuchangia ukatili kwa kundi hilo, baadhi yao baadaye huathirika kisaikolojia.

Akiwasilisha ripoti hiyo jijini Dar es Salaam juzi, mwandishi wa ripoti hiyo, Fundikila Wazambi, alisema asilimia kubwa ya wasichana wanaopitia vitendo vya ukatili, wanakumbwa na tatizo la akili.

Alisema kuwa sheria zisizo rafiki, umaskini, rushwa ya ngono na kutelekezwa vinachangia kwa kiwango kikubwa kuminya haki na ustawi wa wasichana nchini.

Wazambi alisema ukosefu wa mwongozo na usaidizi wa wazazi kwa wasichana hao ni miongoni mwa vikwazo kwa wasichana kufikia malengo yao kielimu na kwamba baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwashawishi watoto wao wasifanye vizuri kwenye mitihani yao.

"Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo, ripoti inalitaka Bunge kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na kuweka miaka 18 kuwa ndiyo umri wa chini wa kisheria wa kuolewa.

"Mapendekezo pia yanajumuisha kuainisha taulo za kike kama mahitaji muhimu na kutekeleza mpango wa utoaji taulo hizo bila malipo kwa wanafunzi shuleni.

"Watoa taarifa muhimu, wakiwamo wataalamu wa masuala ya haki za watoto wa kike, wamehimiza kuondolewa ushuru kwenye taulo za usafi, wakisisitiza kuwa upatikanaji wa bidhaa hizo ni hitaji la msingi kwa wasichana," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, Rebeca Gyumi alisema tathmini hiyo inalenga kutathmini hali ya haki na ustawi wa watoto wa kike nchini, ikilenga elimu, afya na nyingine za msingi.

"Wakati dunia inapojiandaa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike' katika siku zijazo, chini ya kaulimbiu 'Maono ya Wasichana kwa Wakati Ujao', tunasisitiza haja ya haraka ya kuchukua hatua ili kukuza sauti na ndoto ya wasichana kwa ajili ya maisha yao ya baadaye," alisema.

Hellen Kijo-Bisimba ni mwanaharakati mkongwe, alisema ili kulinda haki za wasichana nchini, kuna haja serikali kutekeleza amri ya mahakama kwa kurekebisha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwa kuwa inakwamisha juhudi mbalimbali zinazolenga kukuza utu na maendeleo ya mtoto wa kike.



Mchuuzi wa mboga akizipanga bidhaa zake, wakati akisubiri wateja nje ya Soko Kuu la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ukosefu maji wasababisha kushamiri ukatili kijinsia

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

UKOSEFU wa huduma ya maji katika Kijiji cha Dilifu, Kata ya Magamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi, umesababisha kushamiri vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.

Baadhi ya wanawake wa kijiji hicho waliiambia Nipashe jana kwamba ukosefu wa huduma ya maji umekuwa ukiwafanya wasiaminike kwa wenza wao na wanaporejea kutoka kutafuta maji, wanapokea vipigo kwa waume zao kwa madai wanakwenda kufanya ngono na watu wengine.

"Mimi nilishindwa kuvumilia maana kila kukicha ni kipigo, nikaona bora tuachane tu, kwani ninaamka alfajiri kwenda kutafuta maji, lakini mtu ukimweleza haelewi, ni kipigo kwa madai nimechelewa kurudi nyumbani," alisema Sharifa Ramadhani.

Marry Joshua alisema hali ya upatikanaji maji katika kijiji hicho hasa nyakati za kiangazi ni mbaya na wanawake wengi wanatembea umbali mrefu na wakati mwingine kuchukua muda mrefu kwenye bomba moja lililoko kijijini huko.

"Kijiji kina bomba moja tu, watumiaji maji wapo zaidi ya 5,000, tunasota tangu asubuhi hadi jioni, wakati mwingine ukifika mchana unatoka usiku kutokana na foleni ilivyo kubwa, lakini ukimweleza mume wako hakuelewi, anadai ulikuwa kwa mwanamume mwingine," alilalamika.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mpanda, Agnes Mbalaganya, alikemea vitendo vya aina yoyote vya ukatili dhidi ya wanawake na kuwataka watoe taarifa kwa polisi matukio kama hayo yanapojitokeza.

Akizungumzia utatuzi wa kero hiyo, Mhandisi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Manispaa ya Mpanda, Philipo Pagati, akiri kuwapo ugumu katika kupata maji kijijini huko.

Alisema wako katika mchakato wa kujenga miundombinu ya maji itakayowezesha wananchi kufikiwa na huduma hiyo muhimu.

Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inaelekeza serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama umbali usiozidi mita 400 kutoka katika makazi yao, hivyo kinachoendelea kijijini Dilifu, ni kinyume cha sera hiyo.

# Bashungwa ataka wanaotekeleza miradi kuzingatia usalama kazini

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema wanaohusika katika miradi ya ujenzi, wanatakiwa kuzingatia usalama wa wafanyakazi maeneo ya kazi.

Bashungwa alitoa maelekezo hayo jana alipozungumza na wananchi katika Shule ya Sekondari Msangani, wilayani hapa ambayo ujenzi wake utagharimu Sh. milioni 528.

Akiwa katika shule hiyo, waziri huyo alisema masuala ya usalama kazini yanatakiwa kuzingatiwa kwenye miradi ya ujenzi ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea.

Pia aliagiza viongozi wanaosimamia ujenzi wa shule hiyo kuhakikisha wanakamilisha mapema mwezi ujao ili wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2025 wapate nafasi.

Bashungwa alisema ziara hiyo ni kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo na kueleza wananchi mambo yaliyofanywa na serikali.

Kuhusu barabara kuu ya Chalinze - Morogoro, alisema ufinyu wake unajulikana na ipo mipango ya upanuzi ambayo inaendelea kuwaondolea watumiaji adha ya foleni za mara kwa mara.

Akizungumzia barabara ya Msangani ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami, waziri huyo alimwelekeza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Baraka Mwambage kubainisha madeni ya mkandarasi na kuyafikisha wizarani yafanyiwe kazi.

Bashungwa alisema madeni hayo yakifikishwa yatashughulikiwa haraka ili mkandarasi arudi kazini na kukamilisha eneo lililobaki.

Pia alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), kubainisha barabara zinazosuasua zitafutiwe fedha kwa haraka na kujengwa kuwaondolea adha wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema mkoa huo umeendelea kujimarisha kiuchumi hususani katika sekta ya uwekezaji ambapo zaidi ya viwanda 1,000 vimejengwa, vikiwamo vikubwa zaidi ya 100. Kati yake, 68 vimejengwa wakati wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kunenge alimwomba waziri huyo kufanyia kazi suala la Uwanja wa Ndege Mafia, ili ufanyiwe maboresho na kuwezesha ndege za watalii kutua tofauti na sasa ambapo ndege ndogo pekee ndizo zinatua.

Pia aliomba serikali kuangalia uwezekano wa upanuzi wa barabara kuu ya Chalinze -Morogoro ambayo gari lilipata hitilafu, inasababisha foleni na adha kwa wasafiri wengine wanaotumia barabara hiyo inayotegemewa kiuchumi.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Saimon, alisema kuwa katika uongozi wa Rais Samia, shule za sekondari 10 na zingine 10 za msingi zimejengwa na kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi iongezwe mapambano dhidi ya tatizo la udumavu

**TATIZO** la udumavu kwa watoto nchini limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu huku serikali ikichukua hatua katika kukabiliana nalo kwa kushirikiana na wadau wa ndani na wa nje. Kwa namna linavyozungumzwa linaonesha kuwa bado ni kubwa na lina athari kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mtoto anapodumaa maendeleo yake ya ukuaji yanakuwa ya shida na hata uwezo wake wa kufanya mambo kwa ufanisi, kuanzia darasani hadi kwenye maisha yake ya kila siku, unakuwa mdogo. Kwa mantiki hiyo, mtu kama atakuwa na udumavu tangu akiwa mdogo, utendaji kazi wake utakuwa mdogo, hatakuwa na tija na atashindwa kufanya mambo mengi kwa sababu ya uwezo mdogo wa kufikiri.

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2022 kuhusu udumavu, theluthi moja ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wamedumaa. Takwimu hizo zinaonesha kwamba kati ya watoto watatu, mmoja ana udumavu hali inayoashiria kuwapo kwa hatari ya kuporomoka kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa ufungwaji wa mkutano wa wadau wa lishe nchini uliofanyika Mwanza hivi karibuni, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Jesca Lebba, alisema kwa sasa, hali ya udumavu katika Mkoa wa Mwanza ni asilimia 28, ikiwa imepungua kutoka asilimia 39 mwaka 2018. Hali hii inaashiria mwelekeo mzuri, huku lengo la taifa likiwa ni asilimia 30.

Dk. Lebba, alisema katika mkoa huo, halmashauri zinazokabiliwa zaidi na tatizo hilo ni Ukerewe, Buchosa na Kwimba, lakini jitihada zinafanyika kuboresha hali hiyo. Alisisitiza kuwa mikakati mbalimbali inafanyika ili kupunguza tatizo hilo kwa kuwa wanaamini kwamba lishe ni muhimu kwa maendeleo ya binadamu na bila kuwa na afya njema, mtu hawezi kufanya chochote.

Mtaalamu huyo wa afya alisema tatizo kubwa linalochangia kuwapo kwa hali hiyo ni kukosa lishe bora ambayo inahitaji vyakula kutoka makundi sita. Hali hiyo, alisema haizingatiwi na wakazi wa mikoa huo ambao wengi ni wavuvi na kutokutumia samaki wanaovua badala yake huuza. Pia kwa mujibu wa Dk. Lebba, watu wengi hawatumii mboga za majani na matunda.

Licha ya kuwapo kwa takwimu hizo, inaelezwa kuwa kumekuwa na mafanikio makubwa katika kupunguza tatizo hilo kwa mikoa mitano ya Tanzania Bara kutoka mwaka 2016 hadi 2022 kwa wastani wa asilimia 10. Mikoa hiyo na asilimia kwenye mabano ni Mtwara (15.7), Tanga (14.9), Lindi (13.7), Mwanza (11.1) na Kigoma (10.9).


Pamoja na kuwapo kwa matumaini hayo ya kupungua kwa udumavu, inasikitisha kuona kwamba mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Iringa, Njombe, Mbeya na Rukwa ambayo ni wazalishaji wakubwa wa vyakula ndiyo inaongoza kuwa na tatizo hilo. Sababu kubwa ya kuwapo kwa hali hiyo, kwa mujibu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Tawala za Mikoa ni jamii ya watu wa mikoa hiyo kutozingatia ulaji sahihi wa vyakula.

Ni wazi kwamba serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na tatizo la utapiamlo na udumavu ambavyo vina uhusiano mkubwa ikiwamo kutoa elimu ya lishe kwa wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na shuleni. Pia serikali imeweka suala la lishe kama kipaumbele muhimu katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya taifa.

Juhudi hizo za serikali zinapaswa kupongezwa na kuungwa mkono na wadau mbalimbali zikiwano asasi za kiraia ambazo nimejipambanua katika kupambana na afya ya watu ili kuwa na jamii yenye siha kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Hakuna maendeleo ya taifa lolote yanayoweza kupatikana kama jamii ina tatizo la afya ikiwamo utapiamlo na udumavu, hivyo ili nchi isonge mbele kijamii na kiuchumi katika sekta kama kilimo, viwanda, biashara, ufugaji na uvuvi, jambo la msingi la kuzingatiwa ni kupambana na utapiamlo na udumavu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Wazazi, walezi tunajua wanafunzi wanacheza kamari saa za darasani?

**KILA** mara wazazi na walezi wamekuwa wakitupiwa lawama kuwa chanzo cha watoto wao kukithiri utoro shuleni, watoto wa mitaani na kujihusisha na vitendo viovu kwa kujiunga katika makundi yasiyofaa.

Migogoro ndani ya ndoa, nayo imekuwa ikielezewa kuwa imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la watoto wengi wa mitaani, kukosa mwelekeo kwa kuwa na tabia mbaya na kupata malezi mabaya.

Hayo yote inawezekana kuwa yapo, isipokuwa ni zipo njia za kuhakikisha kwamba hayaendelei kutokea katika jamii kwa kuziba viashiria vyake.

Mbaya zaidi na jambo la kusikitisha ni kitendo cha baadhi ya wanafunzi kuonekana wakizagaa mitaani na kwenye maeneo yasiyofaa kwa ajili ya ustawi wa makuzi yao.

Hapo ndipo baadhi ya watu waliposikika wakilalamika baadhi ya shule kuwa zinachangia wanafunzi kukithiri vitendo vya utoro, kutokana na kurudishwa nyumbani bila ya wazazi na walezi wao kupewa taarifa kwa njia ya barua na simu.

Tangu shule zilipofunguliwa siku chache zilizopita, wanafunzi wengi wameshuhudiwa wakizagaa mitaani wakizurura huku na kule, bila ya kuwa na sababu za msingi.

Wanafunzi wengine wameonekana maeneo ya sokoni 'wakichakura' mabaki ya bidhaa zilizotupwa, wengine wakiwinda ndege kwenye miti kwa kutumia manati na wengine mtoni na mabwawa wakivua samaki.

Wapo waliokutwa wakicheza mpira kwenye maeneo yaliyowazi na majumba makuu ambayo ujenzi wake haujamilika.

Wengine walikuwa wakicheza mchezo wa bao, kamari na mingine katika vichaka.

Kibaya zaidi, wako waliokutwa maeneo zinakoendeshwa biashara za vileo kwenye makazi ya watu, wakipambana kucheza kamari kwenye mashine maarufu kama bonanza. Ni mchezo huo uliokolea kutokana na wanafunzi hao kugawanyika katika timu mbili.

Ni kila upande ulikuwa unashangilia, mmoja unapoliwa na mwingine unapokula fedha ambazo zilipatikana kwa wao kuchangishana.

Kitendo hicho kiliwafanya hata wapita njia katika sehemu hizo za biashara, kusimama kufahamu kulikoni huku wengine wakipigwa na butwaa kutokana na vitendo hivyo kufanyika wakati wanafunzi hao wakitakiwa kuwa shuleni kwa kuwa ni muda wa masomo.

Wanafunzi hao walipoulizwa kulikoni, walisema wameamriwa na walimu kurudi nyumbani kwa wazazi na walezi wao kwenda kuchukua fedha kwa ajili ya kuchangia chakula cha mchana shuleni.

Ni kweli makuzi ya mtoto na malezi bora huanzia kwa mzazi na mlezi nyumbani na anapokabidhiwa shuleni inakuwa jukumu la mwalimu kuhakikisha anapata elimu bora. Chakula cha mchana shuleni kwa mwanafunzi ni muhimu kwa sababu kinasaidia kumjenga katika afya bora, akili na kuwa na usikivu darasani.

Kwa maana hiyo, kamati za shule zingetakiwa kuwasiliana na wazazi na walezi wa wanafunzi ambao hawajalipa fedha kwa ajili ya kuchangia chakula hicho, badala ya kuchukua hatua ya kuwarudisha nyumbani bila ya kuwapa taarifa.

Matokeo yake, wanafunzi hao wamekuwa wakitoka nyumbani asubuhi na kuishia mitaani wakijihusisha na vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikichangia kumomonyoka kimaadili.

Watoto hao wanapoamka asubuhi na kuaga wanakwenda shule, wako wanaopewa fedha kwa ajili ya kununua maji, matokeo yake wanaelekeza katika michezo ya kamari, mchezo ambao kwa mujibu wa sheria hauruhusiwi kuchezwa na vijana wenye umri chini ya miaka 18.

Kwa mujibu wa wanasaikolojia, mtoto anapoanza kuwa na akili ndicho kipindi cha kuanza kumdhibiti kitabia.

Wanasema, akiachiwa katika kipindi hicho, ndipo anapoanza kuiga tabia mbaya na njema. Shime wazazi, walezi na walimu tushirikiane katika malezi na makuzi ya watoto kwa kupeana taarifa wanapokuwa shule na nyumbani.

# Mwanafunzi afanyiwa ukatili, atupwa nje ya nyumba yao

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWANAFUNZI wa kike anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kenyamanyori, Halmashauri ya Mji wa Tarime (16), amelazwa katika Hospitali ya Rufani Kwangwa, Musoma, mkoani Mara baada ya kufanyiwa ukatili na kutupwa katika vichaka jirani na nyumbani kwao.

Binti huyo anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana wakati akienda shuleni kisha kupatikana akiwa amejeruhiwa maeneo mbalimbali ya mwili ikiwamo kichwani.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagote ambaye ni baba mzazi wa mtoto huyo, Maginga James, alisema mtoto huyo alitoweka Oktoba 2, mwaka huu baada ya kwenda shule na jioni kutokurejea nyumbani.

Alisema baada ya kutomwona mtoto wao ilibidi waende shuleni kujua sababu ya binti yao kutokurejea nyumbani baada ya muda wa masomo na kuelezwa kuwa hakufika shuleni siku hiyo.

"Tuliambiwa na walimu kuwa jana hakufika shuleni hivyo tulianza kumtafuta majira ya mchana tulipata taarifa ya kuwapo mwanafunzi wa kike ambaye amekutwa amejeruhiwa hajitambui kichakani," alisema.

Aidha, alisema walipofika walikuta watu wamejaa eneo hilo kisha Polisi walifika na walimtambua ni mtoto wao.

Alisema walipomkagua walibaini ana jeraha kubwa kichwani lililotokana na kuchomwa na kitu chenye ncha kali, pia amejeruhiwa kwenye kidevu, kisogoni, sikio na sehemu nyingine za mwili wake.

"Tulimfikisha Hospitali ya Wilaya Tarime na madaktari walijitahidi kumwekea dripu za maji huku akiwa katika hali mbaya

hajitambui na kupata rufani kwenda Hospitali ya Rufani Kwangwa

Musoma ambako alilazwa kwa siku nne bila ya kujitambua akipatiwa matibabu na Jumatatu (juzi) alianza kupata fahamu," alifafanua James.

Alisema baada ya kupata fahamu aliomba apatiwe uji, awali alikuwa anapatiwa chakula kwa mirija na kwamba wanatarajia akirejesha fahamu zake watajua ni watu gani walimfanyia ukatili huo.

Diwani wa Kata ya Kenyamanyori, Farida Nchagwa alisema tukio hilo katika kata yake yenye machimbo ya dhahabu ya

Kebaga Tagota si la kwanza yamekuwapo mara kwa mara ikiwamo mauaji, vijana kuchomana visu.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuwakamata wahusika waliomteka mwanafunzi huyo, ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia ovu kwa watu wengine. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya SACP Michael Njera, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo

na kusema kuwa wanawahoji watu wawili kuhusiana na tukio hilo na wanaendelea na uchunguzi.

Aliwataka wote wanaoendeleza vitendo vya uhalifu katika eneo hilo na maeneo mengine kuacha mara moja.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, ni kosa la jinai kwa mtu mwanamume kumbaka msichana au mwanamke na adhabu yake ni kifungo cha hadi miaka 30 gerezani au maisha gerezani kulingana na umri wa aliyebakwa au wabakaji walitenda ukatili huo kwa kundi.



Dk. Joseph Sungura wa Hospitali ya CCBRT ya Msasani (kulia), akimpima macho mmoja wa wananchi, wakati wa zoezi la upimaji wa afya ya macho bure linaloendeshwa na hospitali hiyo kwa wakazi wa Tegeta, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani na kufungua kituo cha huduma za macho katika jengo la Kibo Complex Tegeta. **PICHA: JOHN BADI**

KESI YA WANANDOA

# Washtakiwa waomba kuongeza wakili

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeshindwa kuendelea kusikiliza kesi ya tuhuma ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi inayowakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54), baada ya washtakiwa hao kuongeza wakili mwingine wa kuwatetea.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania asili ya kihindi wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana Dar es Salaam, wanatuhumiwa kwa mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21, 2023.

Wakili wa Serikali Faraja Ngukah alidai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo kuwa kesi hiyo iliitwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa na pia wana shahidi mmoja tayari kuendelea.

Baada ya Ngukah kudai hayo, Wakili Mayele alidai mahakamani kuwa washtakiwa wameongeza wakili ambaye ni yeye, kwa hiyo anaomba apewe muda ili aweze kupitia mwenendo wa kesi tangu imeanze hadi ilipofikia.

> **"Lakini yule mama alivyokuwa akionekana pale chini, alionekana kama amefariki dunia, ikabidi atafutwe mwenyekiti wa serikali za mitaa, akasema 'haiwezekani kuvunja mlango ..**

Kutokana na hali hiyo, Mahakama ilikubaliana na ombi la Wakili Gabriel Mnyele na pande zote zilikubaliana kesi hiyo iendelee kusikilizwa siku mbili mfululizo Novemba 6 na 7, mwaka huu, lakini wakili mwingine wa washtakiwa hao, Edward Chuwa, alitaka iwe tarehe sita, tarehe saba ana kesi Mahakama Kuu.

Wakili Ngukah aliiomba mahakama hiyo imwonye shahidi wa tano katika kesi hiyo ili afike tarehe ya kesi kutoa ushahidi wake. Hata hivyo, shahidi huyo alidai kuwa na yeye ataomba udhuru kwa sababu ni mara ya tatu anafika mahakamani hatoi ushahidi amechoka.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hadi Novemba 6, mwaka huu kwa kuendelea kusikilizwa kwa shahidi wa upande wa mashtaka.

Ilidaiwa kuwa Nathwan anatuhumiwa Julai 21, 2023 akiwa eneo la Mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam kinyume cha sheria alimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit kwa kumzamisha kichwa chake kwenye ndoo ya saruji iliyochanganywa.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MAABARA: KUMBUKUMBU NAMBA. REQ-00000610**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha kampuni au mashirika yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma za Maabara katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalosafirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kusafirisha mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na jumla ya Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Katika hatua ya uendeshaji, EACOP Ltd itakuwa na Maabara ndani ya Miundombinu ya Hifadhi ya mafuta ya Baharini ili kutoa huduma ya ainisha ubora wa mafuta ghafi na maji yanayohusiana nayo, Pamoja na mambo mengine ikijumuisha kuangalia Mashapo ya Msingi na Maji (BSW). Ili maabara hii ifanye kazi, kampuni inakaribisha kampuni zenye weledi ambazo zina uwezo wa kiufundi, na rasilimali watu kutoa huduma za uendeshaji wa maabara hii ikiwa ni pamoja na:

- Kutoa mtaalam mmoja aliyehitimu na mwenye leseni kutoka serikalini kwa ajili ya kuratibu utunzaji wa kemikali, usimamizi wa hifadhi za kemikali, huduma za vifaa vya maabara na utoaji ripoti za maabara.
- Kutoa wasanifu wawili wa Maabara kwa ajili ya shughuli za kila siku za maabara ya Tanga na makadirio ya ujazo na gharama zinazohusiana upakuaji wa mafuta .
- Kufanya mjaribio ya ubora , ufanisi na matengenezo ya vifaa vya Maabara ya EACOP.
- Kuwezesha Maabara ya Tanga kupata Ithibati ya ISO 17025 ya kudumu.
- Kufanya usimamizi wa taka za Maabara.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni zinzoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu, na uwezo wa kutoa huduma kwa wigo unaohitajika.
- Maelezo ya shughuli au miradi iliyofanyika inayofanana na huu inayotoa ushahidi na kuwapo kwa timu yenye sifa stahiki, maarifa ya huduma za maabara, na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili na ripoti ya sasa ya taarifa za kampuni toka BRELA (ambatanisha nakala)
- Unashauriwa kuwasilisha Ushahidi wa usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa QHSE, shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vinavyotumika vya ndani na vya kisekta kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa Sera za Kupambana na Rushwa, Kupambana na Rushwa, Uzingatiaji na Haki za Kibinadamu.
- Ujuzi Mtoa huduma wa maabara anapaswa kuwa na ithibati ya ISO 17025.

Makampuni au mashirika ambayo yana uwezo, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma Maombi (EOI) kupitia barua pepe, pamoja na kuambatanisha hati zilizoorodheshwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop. com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) maombi yatumwe kabla au saa **11:00** saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **24 Oktoba 2024**. Kichwa cha barua pepe kitakuwa: **REQ-00000610 Utoaji wa Huduma za Maabara**.
Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote ya kuonesha nia lazima ya andikwe kwa Kingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Mahakama yawaachia huru waliosota gerezani miaka 10

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam imewaachia huru vijana watatu waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya mauaji ya mtoto, Glory Tumani (7), waliosota gerezani miaka 10 tangu mwaka 2014.

Walioachiwa huru ni Baraka Machange, Yasin Omary na Ally Said, ambao walituhumiwa kutenda tukio hilo Oktoka 10, 2014 jijini Dar es Salaam, wakidaiwa kumnajisi mtoto huyo na kisha kumuua na kumtupa porini.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Elizabeth Mkwizu wa mahakama hiyo, alisema mahakama inawaachia huru washtakiwa kwa sababu upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kesi hiyo bila kuacha shaka.

Jaji Mkwizu alisema mahakama baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili, ilijiuliza maswali kadha wa kadha, ikiwamo ni nani aliyewaona watu hao wakiua mtoto huyo.

Pia alisema mahakama haikuelezwa namna ambavyo vielelezo mbalimbali jinsi vilivyohifadhiwa au kupewa namba ikiwamo tofali, mchanga na nguo zilizokutwa eneo la tukio.

Pia alisema ushahidi ulieleza kwamba mama alimwacha mtoto wake Glory na mdada wa kazi anaitwa Fatuma, lakini haikuelezwa baada ya kumwacha Glory alikwenda wapi na aliondoka na nani, lakini pia wawili hao hawakuletwa mahakamani kutoa ushahidi.

Jaji Mkwizu alisema kwa mazingira hayo mahakama inaona ushahidi wa upande wa mashtaka hautoshi kuwatia hatiani washtakiwa, hivyo mahakama inawaachia huru kwa shtaka la mauaji na ambao hawajaridhika na hukumu hiyo wana haki ya kukata rufani.

Hukumu hiyo ilisomwa takribani saa moja na nusu, ikiwatoa machozi wazazi wa mtoto huyo (baba na mama) huku washtakiwa hao wakionekana wenye furaha wakipongezana na ndugu zao.

Upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi tisa na vielelezo na pia washtakiwa wote kila mmoja alikuwa ana mashahidi wawili ambao ni wazazi wao. Inadaiwa wazazi hao walifika kuwatolea ushahidi watoto wao ili kuthibitisha umri wao kwa sababu walikuwa wakionekana wana umri mdogo ambapo waliweza kutoa mahakamani kielelezo cha cheti cha kuzaliwa na kadi za kliniki.

# Wanafunzi watoroka shuleni kwenda kuchenjua dhahabu

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

BAADHI ya wazazi na walezi wilayani Mpanda, mkoani Katavi wameiomba serikali kuchukua hatua kukabili utoro wa wanafunzi shule za jirani na maeneo ya machimbo ya madini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hizi kuhusu tatizo linalojitokeza katika maeneo ya machimbo ya madini ya Ibindi, Halmashauri ya Nsimbo wilayani Mpanda mkoani hapa, mmoja wa wachimbaji wadogo, Anastazia Peter alisema serikali inapaswa kuchukua hatua kukomesha vitendo vya utoro kwa wanafunzi hasa wa Shule ya Msingi Ibindi ambao wengi wao nyakati za asubuhi huenda kutafuta dhahabu maduarani na mtoni badala ya kuwa darasani.

"Ukija hapa siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa utajionea watoto wa Shule ya Msingi Ibindi wakiwa wamejaa humu mtoni wakichekecha...ili kutafuta mabaki ya dhahabu na wazazi wao hawana habari wala hawafuatilii maendeleo ya watoto wao shuleni," alisema Anastazia.

Rafaeli Sila, mwalimu wa darasa la saba shuleni hapo, alisema kuwa tatizo la watoto kuacha masomo na kwenda machimboni ni kubwa hasa nyakati za masika, mathalani kwenye darasa lenye watoto 100 ni kawaida kwa watoto 30 hadi 40 kutohudhuria shuleni kwa sababu ya kwenda kwenye utafutaji wa dhahabu.

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusuph, akiwa katika Kijiji cha Dilifu ambacho nako kuna shughuli za uchimbaji wa madini ambako inadaiwa kuwa utumikishwaji wa watoto kwenye shughuli hizo umekithiri, alipiga marufuku vitendo hivyo na kuagiza mamlaka kuhakikisha watoto wote wanaondolewa katika machimbo na kurejeshwa shule.

# KCB yapanda miti mikoa minane kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja

**INATOKA UK, 1**

mikoa mbalimbali ya uendeshaji wake nchini.

Wakati wa hafla hiyo, Machango alitoa shukrani kwa Shule ya Msingi Mbagala Annex, moja ya wanufaika wa mpango huo kwa kuipokea KCB Bank kwa moyo mkunjufu katika juhudi hizo muhimu ya kuhifadhi mazingira.

"Dhamira yetu inakwenda zaidi ya mafanikio ya kibiashara; tumejikita katika uhifadhi wa mazingira. Leo hii, tunajivunia kupanda zaidi ya miti 1,500 katika shule mbalimbali zilizoko Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Zanzibar, Geita, Kahama, Mwanza na Morogoro," alisema Machango.

Naye Ruth Mussa, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Mbagala Annex, alitoa shukrani zake kwa KCB Bank kwa kushiriki katika mpango huo, huku Ofisa Mazingira wa Manispaa ya Temeke, Phina Bernad, akiipongeza benki hiyo kwa mchango wake mkubwa na kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha miti iliyopandwa inatunzwa ipasavyo.

KCB Bank inatoa wito kwa jamii na mashirika kushirikiana katika kuendeleza juhudi za kuhifadhi mazingira na kufikia maendeleo endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.



# Afa kwa kubakwa, kutobolewa jicho

Na Jaliwason Jasson, BABATI

WATU wasiojulikana wanadaiwa kumbaka, kumwingilia kinyume na maumbile na kumtoboa jicho mwanamke, Mkazi wa Magugu wilayani hapa Mkoa wa Manyara na kufariki dunia.

Mwanamke huyo ambaye jina lake halijatambuliwa, alikutwa katika eneo la Kijiji cha Matufa, Kata ya Magugu, akiwa hajitambui kutokana na hali yake kuwa mbaya.

Kaimu Kamanda wa Polisi Manyara, Lucas Mwakatundu, alisema hana taarifa za tukio hilo na kuahidi kutoa ufafanuzi baada ya kuwasiliana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Babati.

Wakizungumzia tukio hilo, baadhi ya viongozi wa siasa na wakazi wa eneo hilo, walidai lilitokea Oktoba 5, mwaka huu.

Kati ya Januari hadi Agosti mwaka huu, Manyara kumeripotiwa kuwa na matukio 6,261 ya ukatili wa kijinsia, ikiwa ni ongezeko la matukio kama hayo 2,099 yaliyotokea kwa kipindi kilichopita.

Mbunge wa Babati Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, akizungumza na wakazi wa Magugu, alisema vitendo hivyo vinasikitisha, kutia aibu na havistahili kuvumiliwa, hivyo ni vizuri utu wa mtu kuheshimiwa na kuvitokomeza.

Aliwaomba viongozi wa dini, mila na wananchi kukemea vitendo vya ukatili vinavyoendelea katika mkoa huo na kutokomezwa.

**"Kwa kushirikiana na wananchi, tulimkamata kijana mmoja anayetuhumiwa kuhusika na tukio hilo (jina limehifadhiwa) na tulimkabidhi Polisi," alisema Naomi.**

Vilevile, aliwaomba wananchi kufichua uhalifu huo na mwingine kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola ili wanaohusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za sheria zichukuliwe dhidi yao.

Awali, Diwani wa Viti Maalum, Naomi Richard, alisema baada ya kupata taarifa za tukio hilo kwa kushirikiana na wananchi walifanya msako dhidi ya waliofanya unyama huo na kumkamata mmoja.

"Kwa kushirikiana na wananchi, tulimkamata kijana mmoja anayetuhumiwa kuhusika na tukio hilo (jina limehifadhiwa) na tulimkabidhi Polisi," alisema Naomi.

Alisema kabla ya kufikwa na umauti, hali ya mwanamke huyo ilikuwa mbaya na kwamba alikufa wakati madaktari wakifanya jitihada za kuokoa uhai wake.

Wiki iliyopita, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa mkoa huo, Anna Fisoo, aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa jeshi kutokana na matukio mengi ya ukatili kusuluhishwa kifamilia na kuwakosesha haki waathirika na kusababisha kukithiri katika jamii.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka mfumo wa afya wa kutolea taarifa zilizowasilishwa Agosti mwaka huu, matukio 6,261 ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yaliripotiwa na kwa mwaka jana yalikuwa 8,360.




Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, SSP Hadija Sokolo (kulia), akijadiliana jambo na Mkuu wa Kituo cha Polisi Muheza, SP Kuruthum Bambe katika Uwanja wa Jitegemee juzi, baada ya kutoa elimu kwa vijana kushiriki ulinzi shirikishi. Kushoto ni Ofisa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa wilaya hiyo, Msafiri Nyaluva. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Taarifa maafa Hanang' hadharani

Na Jaliwason Jasson, HANANG'

SERIKALI imetoa taarifa ya tathmini ya jiolojia, haidrolojia na mazingira ya maafa yaliyosababishwa na maporomoko ya Hanang' mkoani Manyara na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 89 na majeruhi 139.

Maafa hayo yalitokea Desemba 3, mwaka jana yaliacha madhara makubwa ya uharibifu wa makazi, miundombinu na upotevu wa mali.

Akizungumza jana wakati wa kupokea taarifa ya tathmini hiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Jiolojia kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini nchini (GST), Dk. Ronald Massawe, alisema Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kutokea maafa hayo iliunda Tume ya Utafiti kutoka GST na vyuo vikuu ili kubaini chanzo cha maafa hayo.

Dk. Massawe, alisema tume hiyo katika utafiti wake ilibaini kuwa mlima huo, ulitengeneza maeneo dhaifu na kumeguka kutokana na kushindwa kuhimili maji wakati mvua zinanyesha.

"Miamba ilichanganyika na ikahifadhi maji na hivyo maji yaliyokuwa yamejihifadhi yalitoka ndio yakatengeneza tope," alisema.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, alisema serikali itaendelea kuimarisha menejimenti ya maafa ili kukabiliana na matukio hayo nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Yonazi, ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa kwa ufanisi, serikali kupitia ofisi yake na wadau, imeendelea kuboresha utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa nchini kwa kuandaa nyaraka zinazoainisha majukumu ya msingi kwa wadau na kutoa mwongozo wa majukumu kwa wadau.

Desemba 7, mwaka jana, GST ilieleza kwamba katika tukio hilo hakukuwa na tetemeko la ardhi wala mlipuko wa volcano katika mlima huo.

Maeneo yaliyoathirika zaidi ni ya mji mdogo wa Katesh na kata zake za Jorodom na vitongoji vyake vya Udameseki, Gawal na Jorodomu Kati.

Kata ya Gadang'a na vitongoji vyake vya Gadang'a A, Gadang'a B na Kata ya Katesh A na Gedang'ongyi na Katesh, vitongoji vya Kates Stendi na Katesh B.

Kwa upande wa Kata ya Gendabi, Kijiji cha Gendabi katika vitongoji vya Uhuru na Dumanang'.

# Ujenzi maabara TEHAMA 4,000 sekondari waanza

Na Godfrey Mushi, MOSHI

SERIKALI imeanza ujenzi wa maabara za kisasa 4,000 za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini ili kukabiliana na changamoto ya mafunzo kwa vitendo, vitabu na walimu hususani wa masomo ya sayansi.

Hatuo hiyo ya serikali kuanza kutekeleza ujenzi wa maabara hizo za TEHAMA, inalenga kuongeza uelewa na ufaulu wa wanafunzi wa shule zake za sekondari nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA Tanzania (ICT), Dk. Nkundwe Mwasaga, aliyasema hayo jana mjini hapa Mkoa wa Kilimanjaro kabla ya kuzindua maabara ya kisasa ya TEHAMA ya Shule ya Sekondari ya Manushi.

Dk. Mwasaga ambaye alikuwa ameongozana na Mwenyekiti wa Bodi ya ICT,

Profesa Leonard Mselle, alisema maabara hizo, zitatoa chachu kwa wanafunzi kupata ujuzi, ubunifu, kufanya tafiti na kujifunza ujasiriamali wa kidigitali utakaowasaidia kujiajiri baada ya kumaliza masomo yao.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Teknolojia ya Qsoft Tanzania, Amali Bahanza, alisema mfumo huo wa TEHAMA katika shule nchini, kama sehemu ya dunia hatuwezi kuacha kujijengea uwezo katika kuelekea uchumi wa kidigiti.

Zaidi, alisema ni wajibu wa taifa kuona fursa zilizoko katika tasnia hiyo na dunia nzima inaelekea wapi.

Mkuu wa Shule hiyo, Khamisi Mbawa, alisema moja ya mambo yanayoikabili shule yake ni pamoja na wanafunzi wa kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 12 kwenda na kurudi nyumbani kila siku.

"Hatuna bwalo la chakula, jambo ambalo linasababisha wanafunzi kulia chakula madarasani na nje ya madarasa.

Pia hakuna hosteli (daharia) hizo na kusababisha wanafunzi wa kike kukatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito," alisema.





# Wajawazito wapatiwa msaada

**Na Rose Jacob,**
MWANZA

WADAU wa Afya wa Shirika la The Desk and Chair Foundation wametoa msaada wa vifaa kwa wajawazito zaidi ya 100 kwa ajili ya kujifungua na ujenzi wa shimo la kuhifadhia kondo la nyuma la uzazi katika Kituo cha Afya Makongoro kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 5.4.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo juzi, Mwenyekiti wa Shirika hilo, Sibtain Meghjee, alisema lengo ni kuboresha huduma za uzazi kwa wakazi wa Wilaya ya Nyamagana, Sengerema na Misungwi na kudhibiti vifo vya mama na mtoto.

Meghjee, alisema msaada huo umetolewa na makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na la Nudba la Kanada vifurushi 70 na Angel wa Kanada 30.

Alisema vilevile wametoa zaidi ya mifuko 700 ya vifaa vya uzazi kwa wajawazito ili wasipate shida wakati wa kujifungua katika kituo hicho.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Emma Maneno, alisema ujenzi wa shimo hilo utaboresha usafi wa mazingira ya kituo.

"Kituo cha Afya Makongoro kinahudumia wagonjwa kati ya 250 hadi 300 kwa siku, na kina uhaba wa mabenchi 30, kompyuta 15 na vifaa vingine vya matibabu vitakavyosaidia kuboresha huduma ya uzazi na usalama wa mama na mtoto," alisema.

Diwani wa Mirongo (CCM), Hamidu Seleman, alisema kituo hicho kimetengewa na serikali Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuboresha mazingira na huduma zake.

Alisema mabenchi 30 ya kukalia wagonjwa yako ndani ya uwezo wake na kwa upande wa kompyuta 15 na mashine ya alama za vidole, atatafuta msaada kwa kushirikiana na wadau ili kukiweka kituo katika mazingira bora ya kutoa huduma.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Dk. Furaha Mwakafwila, alisisitiza umuhimu wa wadau kuendelea kushirikiana na serikali kuboresha huduma za afya, hasa kwa wajawazito.

# Ndejembi ashtukia upigaji fedha za miradi

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, amesema kukwama kwa ujenzi wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani kunatokana na baadhi ya watumishi kujihusisha na wizi.

Ndejembi alitoa kauli hiyo juzi wakati akikagua ujenzi wa Kituo cha Afya Segese.

Alisema baada ya kufuatilia ujenzi wa kituo hicho, alibaini mapungufu na kutumika kama mianya ya baadhi ya watendaji kuiba fedha za mapato ya ndani ya serikali.

Alitaja baadhi ya mapungufu hayo kuwa kituo hicho kukosa 'kolido' za kupita wagonjwa, maji, umeme na watumishi ili kianze kutoa huduma kwa wagonjwa.

Alitoa mwezi mmoja kuhakikisha kituo hicho kinaanza kutoa huduma kwa wananchi.

Kuhusu watumishi, aliagiza waazimwe kutoka zahanati na vituo vya vyenye watumishi wengi ili wawahudumie wananchi hasa wajawazito na watoto.

**Kuhusu watumishi, aliagiza waazimwe kutoka zahanati na vituo vya vyenye watumishi wengi ili wawahudumie wananchi hasa wajawazito na watoto.**

Awali akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Msalala Dk. Sisti Mosha, alisema ulianza Oktoba mwaka 2022 na kukamilika mwaka jana kwa gharama ya Sh. milioni 470 kutoka mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

Dk. Mosha, alisema ujenzi wa kituo umekamilika kwa majengo ya wagonjwa wa nje (OPD), maabara, upasuaji na mama na mtoto.

Alisema pamoja na majengo hayo kukamilika, kituo hicho kimeshindwa kuanza kutoa huduma kwa ukosefu wa umeme, maji na watumishi.

Alisema kituo hicho chenye uwezo wa kuhudumia wagonjwa 360,000, kimepokea vifaa tiba vyenye thamani ya milioni 123.

Mkazi wa Kata ya Segese, Angle Deus, amelalamikia kukosa huduma za matibabu na upasuaji kwa wajawazito licha ya ujenzi wa kituo hicho kukamilika.

Angle, alisema wamekuwa wakitembea zaidi ya kilomita 50 kufuata huduma Kituo cha Afya Bugarama, Hospitali ya Ntobo na Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Tatu Ngelela, alisema zahanati iliyopo inakabiliwa na msongamano wa wagonjwa hususani wajawazito na kuwa endapo kituo hicho kingekuwa kinatoa huduma kingepunguza adha hiyo na ya kufuata huduma za uzazi mbali.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Annamringi Macha, aliwataka makandarasi kufuata sheria ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati.

**Imeandaliwa na Shaban Njia na Neema Sawaka (KAHAMA).**



Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Christopher Ngubiagai, wilayani humo, mkoani Mwanza jana, kabla ya kukimbizwa katika kata 11 kwa kuzindua, kuweka mawe ya msingi na kukagua miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 78.8. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# WMA yasisitiza kuwasaka 'wanaochezea' mizani

**Na Alphonse Kabilondo,**
GEITA

WAKALA wa Vipimo Tanzania (WMA) mkoani hapa umesisitiza utaendelea kufanya msako wa kushtukiza wa wafanyabiashara wa vituo vya madini mkoani humo ili kuwabaini wanaokiuka sheria kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Meneja WMA wa Mkoa wa Geita, Eva Ikula kwenye maonesho ya saba ya kimataifa ya madini yanayofanyika katika Viwanja vya EPZA Bombambili.

Eva, alisema msako huo ni mwendelezo wa misako ya kushtukiza katika maeneo ya biashara za madini ili kubaini usahihi wa matumizi ya mizani.

"Ukaguzi wetu hufanywa kushtukiza katika masoko 10 yaliyopo hapa Geita ya Geita Mjini, Katoro, Chato, Lwamgasa, Nyarugusu, Mbogwe, Bukombe, Nyang'wale, Mgusu Nyakagwe, pia na masoko mengine nchini," alisema.

Aliwataka wadau wa sekta hiyo kuhakikisha wanatumia mizani iliyohakikiwa na WMA ili kutambua uzito halisi wa madini yanayonunuliwa na kuuzwa.

Eva, alisema baada ya uhakiki wa mizani, zinawekwa alama maalumu kuonesha utambuzi kuwa inafaa kutumika katika biashara za madini.

"Alama zinazowekwa katika mizani iliyohakikiwa ni stika na lakiri ambayo ina kuwa na alama ya nembo ya taifa pamoja na tarakimu mbili za mwisho za mwaka husika mfano 24 ikiashiria imehakikiwa 2024," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara katika Soko Kuu la Dhahabu Geita, Patrick Charles, aliwakumbusha wafanyabiashara wenzake kuhakiki mizani zao ili kupata haki kama wauzaji na wanaowauzia.

AFYA

## KAACHA KUONA ANA WIKI TATU CHUO KIKUU...

# Rukia; kapoteza fani mazingira, kanasa utangazaji

- Kalala anaona, kaamka haoni, mwisho wake SUA
- Asimulia umaskini unavyokwamisha tiba yake


**Na Beatrice Moses**

"PENYE njia pana njia," ni msemo unaothibitishwa na Rukia Mohamed, kijana aliyekumbwa na mkasa wa ulemavu, hata akashindwa kuona wiki tatu tu baada ya kuanza masomo Shahada ya Kwanza ya Sayansi Mazingira, katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) mwaka 2021.

Ni tukio liliomwachia wakati mgumu akitaka tamaa kimaisha, hasa alipofikiria njia panda ya kuendelea na masomo yake.

Hata hivyo, leo hii Rukia ni mwanafunzi wa mwaka wa pili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC), zao la jitihada na kutokata tamaa.

Anataja mbadala wa teknolojia ya kisasa ya mawasiliano, ilimpa mwanga mpya kuwa na nafasi ya kuendelea na masomo hayo, ingawa amelazimika kubadili fani kutoka mwana- mazingira hadi dira kuwa mtangazaji kwenye vyombo vya habari.



Ni mweledi na anamudu stadi za taaluma yake. Rukia Mohamed, akitumia kompyuta mpakato yake. **PICHA: BEATRICE MOSES.**

**MKASA ULIVYOKUWA**

Rukia ambaye sasa yuko katika mafunzo kwa vitendo katika ofisi za Chama cha Waandishi Wanawake (TAMWA), Dar es Salaam, Nipashe imemshuhudia akifanya mafunzo ya vitendo kwenye mfumo wa mtandao 'Online' akiwa na sauti nzuri, pia uwezo bora wa kuelezea jambo.

Anasimulia alikotoka kwamba, zilikuwa wiki tatu zinakamilika tangu kuanza masomo (mwaka wa kwanza) SUA, siku hiyo alijikuta anachelewa kuamka pasipo kutarajia, kila alipofumbua macho akabaki anaona giza.

Akahisi bado hakujakucha hadi mwanafunzi wenzake alipogonga mlango wake kumuuliza kulikoni bado amelala, Rukia anamsimulia mwandishi katika ofisi za TAMWA, kwamba:

"Nikamwambia mbona naona bado hakujakucha, baada ya kuamka nikagundua kwamba macho yangu ndiyo yamepoteza uwezo wa kuona. Nikaanza kulia, akanisaidia taarifa zikapelekwa kwa uongozi wa chuo, nikaruhusiwa kuondoka kwa ajili ya matibabu."

Anaeleza awali kabla ya kukumbwa na tatizo hilo, alikuwa na changamoto kushindwa kuona mbali, hivyo alikuwa anavaa miwani iliyomsaidia kumudu kuona vyema.

Hivyo, baada ya tukio hilo akarejea nyumbani kwao Dar es Salaam, akapokelewa hospitalini kuchunguzwa na daktari, aliyemjulisha kuwa 'retina' (ngozi ya jicho) ndiyo imeachia, anatakiwa kufanyiwa upasuaji kwa gharama shilingi milioni 4.8.

Rukia anasema ilikuwa kubwa kwao na hawakuweza kuipata wakati huo, hasa alikuwa anamtegemea mama yake, ambaye hakuwa na kipato cha uhakika. Baba yake alishafariki tangu mwaka 2018.

Kijana huyo anasimulia baada ya kupoteza uwezo wa kuona, mama yake alidumisha ukaribu naye, kumsaidia wakati wote, hivyo akapambana kuuza baadhi ya vitu vyake upasuaji ufanikiwe.

Ni upasuaji uliokuwa na hatua tofauti hadi kukamilika. Awali alianza kuona mwanga, giza na mtu akiingia ndani anamtambua kimaumbile, siyo sura halisi, kwa sababu aliona ukungu.

"Kwa watu niliowatambua, hata asipozungumza natambua huyu ni nani. Baada ya miezi kadhaa, hali ilibadilika upande nikawa naona giza nikarejea tena.

"Daktari alinieleza kuwa mafuta yametumika kuweka hiyo retina yalikuwa mepesi, maji ya jicho yalifanya yalainike zaidi na kuyatenganisha, hivyo nilipaswa kufanyiwa upasuaji wa pili," anasema.

Rukia anafafanua gharama yake ilikuwa shilingi milioni 2.8 na baada ya 'kuwalilia' madaktari walipunguza hadi shilingi milioni 2.5 milioni, japo anakiri ilikuwa changamoto kuipata.

Rukia anaielezea Nipashe namna mama yake aliungana na dada yake, pia bibi mzaa mama wakauza baadhi ya vitu, ndipo fedha ikapatikana akafanyiwa upasuaji tena.

Hata hivyo, anasema awamu hiyo haikuwa na mafanikio, akieleza: "Upasuaji wa pili ulikuwa Mei mwaka jana, nilipata maumivu ya kichwa ya mara kwa mara hadi Septemba ndipo presha ikashuka na kuwa ya kawaida."

Anaeleza daktari wake baada ya uchunguzi, akamwambia kuwa 'retina' ilishika vizuri baada ya upasuaji, lakini presha ya macho imesababisha mishipa ya fahamu kushindwa kutafsiri ipasavyo.

Rukia anasema katika matibabu yake, aliambiwa anaweza kupona akienda kutibiwa nje ya nchi kwenye vifaa vya teknolojia ya juu ya utabibu, lakini akakwama gharama kubwa, wamejaribu kuomba

Inaendelea Uk. 13

## SIKU SITA ZA KILA MKOA WANAOFIKIA, WAACHA UJUZI NA KUOKOA VICHANGA

Inatoka Uk. 11

Dk. Rubeja anasema wamefanikiwa kuwagundua watoto wenye changamoto na kuweza kuwapa rufani kwenda hospitali za juu kupatiwa matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya Nkasi, Dk. Thomas Ndeule, anasema ujio wa madaktari hao umekuwa wa manufaa kwa wananchi Nkasi kupata huduma za kibingwa wilayani hapo.

"Pasingekuwa na uwepo wa madaktari Bingwa wa Rais Samia tungelazimika kuwapa rufani wazazi wa watoto hawa kuwasafirisha kuwapeleka katika Hospitali ya Rufani," anasema.

Mkazi wa Nkasi, Anastazia Benedikto, kwa niaba ya wenzake anamshukuru Rais kwa kufanikisha uwapo wa madaktari hao bingwa katika makazi yao.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko mnamo Oktoba, 7, wakati anazindua kambi ya Madaktari Bingwa wa Samia, kuhudumia hospitali tano za mkoa huo na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya katika hospitali hizo, akatamka:

"Nendeni mkatoe hamasa kwa wananchi kuwa na utamaduni wa kupima afya zao kabla ya kuugua, ili kujua hali za afya zao na kupata matibabu sahihi kabla ya tatizo kuwa kubwa na kuleta athari kubwa wakati wa matibabu."

Pia, akashauri uhamasishaji wajawazito kwenda kwenye vituo vya kutoa huduma za afya mapema kuanza kliniki kwa wakati, kuepuka baadhi ya matatizo yanayoweza kutokea wakati wa ujauzito.

"Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa aliofanya katika sekta ya afya, hasa kwa kuona umuhimu wa kusogeza huduma za kibingwa na bingwa bobezi karibu na wananchi na kuleta tija ya kutotumia gharama kubwa kufuata huduma hizo," anatamka Mkuu wa Mkoa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Dk. Jonathan Budenu, anasema kambi hiyo ya madaktari bingwa, itatoa huduma za kibingwa kwa siku saba na kutoa ujuzi kwa wataalamu wa afya walipo katika hospitali tano, ambazo mabingwa wanaenda kutoa huduma.

**NDANI YA KIGOMA**

Wiki hii Jumatatu, jumla ya madaktari bingwa 57 wa Rais Samia wamewasili mkoani Kigoma kutoa huduma za kibingwa kwenye halmashauri zote za mkoa kwa muda wa siku sita na wamepokewa na Katibu Tawala, Hassan Rugwa.

Akiwakaribisha kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Thobias Andengenye, akafafanua katika utashi na nadharia ileile ya Katavi, kutoa huduma kibingwa na kuwajengea uwezo wataalamu wa mkoani humo, akizitafsiri kuokoa maisha ya watu.

Rugwa anasema, huduma hiyo inatolewa kwa ushirika wa Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, lengo ni kuboresha huduma na kupunguza vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi. Pia, inagusa huduma jumuishi za kibingwa Kigoma.

Mratibu wa huduma hizo za madaktari bingwa mkoani Kigoma, Jackline Ndanshau, anasema mkoani himo zipo huduma hizo ngazi ya halmashauri.

Anataja mradi husika una mafunzo elekezi kazini kwa watoa huduma za afya, kuimarisha ubora wa huduma za afya katika hospitali wanazopelekwa Madaktari Bingwa wa Rais Samia.

Mganga Mkuu wa Mkoa Kigoma, Damas Kayera, anasema ugeni wa madaktari bingwa Kigoma, ni furaha kwa wananchi kuhudumiwa kibingwa kwa waliyopaswa kufuata mbali, ikiwamo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Aidha, anasisitiza hamasa ya wananchi kupata lishe bora na sahihi kwa watoto wadogo, vijana, rika la kati na wazee, kulingana na maelekezo ya wataalamu wa lishe katika maeneo yao.

Anasema, ni hamasa inayowasaidia wananchi kujitambua mapema kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kuanza uchunguzi na matibabu mapema, kabla ya tatizo kuwa kubwa.

**MKOANI TABORA**

Katibu Tawala wa Mkoa huo, George Mboya, wakati wa hafla ya mapokezi Madaktari Bingwa Samia mkoani Tabora, Jumatatu wiki hii wakitarajiwa kuwapo hadi Jumamosi ijayo, anasema magari ya matangazo yameunguka kunadi uwapo wa huduma hiyo.

Katibu Tawala akatumia fursa hiyo kumshukuru Rais kuelekeza zaidi ya shilingi bilioni 29.3 kwenye uimarishaji wa miundombinu ya afya na vifaa tiba.

"Ujio wenu unazidi kutuonyesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anatupenda, maana baada ya kutuimarishia miundombinu, ameamua kutushushia huduma hadi ngazi ya za msingi," anatamka Mboya, akiwataka watumishi wa afya mkoani kuwapa ushirikiano.

Mboya, pia amewataka watumishi wa afya katika mkoa huo na wananchi kwa jumla, kuwapa ushirikiano madaktari bingwa waliopangwa kwenye mkoa wao.

Mkurugenzi wa Afya ya Uzazi kwa Huduma za Mama na Mtoto, Dk. Felix Bundala, anasema hilo linafanyika, ikiwa ni matokeo ya mafanikio ya awamu ya kwanza.

Timu hiyo, ambayo huzunguka katika mikoa mbalimbali, kwa ratiba ya siku sita za kuhudumia kila mkoa, hivi karibuni wamekuwa katika mikoa ya Songwe na Singida.

AFYA

# Kula parachichi, ujue unavuna mambo haya...

Na Mwandishi Wetu

UMAARUFU wa parachichi, unatajwa ni kutokana na umbile lake nyororo, laini na ladha isiyo ya kawaida. Parachichi ni tunda lililoko katika kundi la familia ya mdalasini. Kuna aina kadhaa ya parachichi, kuanzia ukubwa, rangi na muundo.

Yote yanakuwa na asili kuendana na hali ya hewa ya kitropiki na yanapovunwa, ni nyororo na laini kama siagi, hata kuwa maarufu sana katika kila kitu kuanzia kwenye kuchanganyia kwenye mlo, mpaka kula baada ya chakula.

Ikianziwa na juisi yake, mpaka inapoliwa kama tunda, mara nyingi inajulikana chakula chenye afya. Mtaalamu wa lishe aliyesajiliwa Taasisi ya Jo Lewin, ana ufafanuzi wake, akiwa na orodha ya faida.

FAIDA ZA PARACHICHI

Sehemu yake ina mgawanyiko wa parachichi na una: protini gramu sita (6); mafuta gramu tano (5); wanga gramu sita (6); potasiamu miligramu 360; na Vitamini E, miligramu 56.

Faida zake zinagawanyika katika orodha kadha:

Kwanza, parachichi linatajwa kuwa chakula chenye virutubisho vingi. Parachichi, pia ni chanzo bora cha mafuta na ina Vitamini E ndani yake, ikiwa chanzo kizuri cha virutubishi. Pia, hutoa nyuzinyuzi nyingi zaidi kuliko matunda mengine, ndani yake kukiwapo madini muhimu kama chuma, shaba na potasiamu.

Pili, tunda hilo linatajwa kuwa na msaada kwa afya ya moyo, parachichi lina mafuta mengi huku asilimia 60 yakiwa ni asili, ambayo utafiti unapendekeza kusaidia kulinda magonjwa ya moyo na kupunguza shinikizo la damu.



Tatu, ni chanzo bora cha potasiamu, virutubishi na nyuzi, ambavyo vyote hunufaisha moyo na mfumo wa moyo na mishipa.

Inaweza kusaidia kupunguza lehemu inayotolewa na parachichi pamoja na asidi ya mafuta ya mbegu. Mafuta hayo ambayo hayajajazwa, hupendekezwa kama sehemu ya lishe bora kusaidia kudhibiti lehemu(cholesterol).

Nne, hilo parachichi linaweza kusaidia kudhibiti hamu ya kula, ikiwa na kalori nyingi zaidi kuliko matunda na mboga nyinginezo.

Hata hivyo, uchunguzi wa kuvutia umeonesha kuwa mafuta ya parachichi husababisha hisia za shibe ambayo husaidia kudhibiti hamu ya kula.

Tano, zao hilo la parachichi linaweza kusaidia kuweka macho yenye afya kando na faida zilizotajwa hapo juu, ikiwa chanzo kikubwa cha Vitamini E ya kinga, pamoja kusaidia macho yenye afya.

**USALAMA WAKE**

Baadhi ya watu wanaweza kupata mzio wa parachichi. Hii ni pamoja na mizio kwenye mdomo ambayo inaweza kusababishwa na athari za nadra.

Parachichi, pamoja na matunda kadhaa ikiwamo matunda kama tufaha, yana kemikali za asili zinazoitwa 'salicylates'.

Baadhi ya watu wanaweza kupata athari ya mzio ikiwa ni pamoja na upele wa ngozi na uvimbe.

- ***Ni elimu ya habari, ambayo undani wake inapatikana katika vituo vya huduma za afya.***

***Kwa mujibu wa BBC.***

# RUKIA; KAPOTEZA FANI MAZINGIRA, KANASA UTANGAZAJI

Inatoka Uk. 12

msaada wa kuchagiwa fedha, lakini hakufanikiwa.

Baada ya kubaini haki hiyo, akaamua kutafuta uwezekano wa kurejea masomoni, changamoto ikawa kutojua lugha ya maandishi ya 'nukta nundu' inayotumiwa na wasioona.

Pia, ni wakati alilazimika kwenda SUA kuomba kuhairisha muhula wa masomo, alikojibiwa isingewezekana, pia hata suala la kumhamisha ikawa ni changamoto, kwa sababu hakuwa na matokeo yoyote ya mitihani chuo haponi, hakuwahi kuifanya.

Rukia anasema katika harakati zake kutafuta suluhisho aendelee na masomo, akafika katika Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM), alikokutana na anayetambulisha kwa jina moja la Mhando, aliyesimulia mkasa wake, akimpa taarifa zenye matumaini.

Anasema, Mhando alimweleza Chuo Kikuu cha Dar es Saaam (UDSM), wangempokea na nafasi ya kuendelea kimasomo, kwa sababu kuna kitengo maalum kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum, hivyo akampa namba za simu za watu wawili awasiliane nao kufanikisha hatua hiyo.

"Nilipompigia mtu wa kwanza alikuwa ni mwanamke, alijibu kwa kifupi kuwa hawezi kunisaidia, hakuna utaratibu wa kuhamishwa bila kuwa na matokeo," anasimulia, akiitaja ni jibu lilikomkatisha tamaa, hata azma ya kumpigia simu mtu wa pili.

Rukia anasimulia kwamba, mdogo wake alimtia moyo kujaribu kuwasiliana na mtu wa pili, aliyemtaja kwa jina Dk. Lucas Kija, akinena, alivyokutana na faraja:

"Alizungumza nami kwa upendo, huku akinifariji kwamba kama nina nia ya kusoma, basi niondoe hofu. Akanielekeza namna nzuri ya kufuata utaratibu wa kuhamishiwa UDSM, huku akinitia moyo kuwa hata kama sina matokeo ya kuonyesha, hiyo inatokana na yaliyoikuta hivyo nisaidiwe, kweli nilifanikiwa."

**AANZA KUJITEGEMEA**

Rukia anaeleza akaanza kwenda kuhudhuria masomo ya awali kujifunza kutumia kompyuta kwa kuwa hakujua kutumia 'nukta nundu'.

"Nilijifunza kwa bidii, baada ya kufanikiwa kujua kutumia alimwomba mama yake amnunulie, akimjulisha kuwa tayari ameweza kuwasiliana hadi kuandika ujumbe wa maneno au kumpigia simu.

"Mama alifurahi aliniambia nimtumie 'sms', nilipomtumia alifurahi sana. Kwangu simu na kompyuta vinanisaidia katika masomo yangu.

"Pia, nafuatilia mambo yanayoendelea ulimwenguni kwenye mitandao ya kijamii ili kupata taarifa muhimu, pia napata burudani kwa kusikiliza vichekesho mbalimbali," anasema.

Msomi huyo anaeleza mbali na kumudu teknolojia, mama yake amemsaidia kumudu maisha ya kujitegemea, akimwongoza kufanya shughuli mbalimbali, ikiwamo kupika, kukata mboga, usafi, ikiwamo kupiga deki au kufua mwenyewe.

Meneja wa Kituo cha Kuhudumia Wenye Mahitaji Maalum UDSM, Dk. Sara Kisanga, anasema Rukia alipokewa na kuanza kupewa ushauri wa kisaikolojia, kumfanya akubaliane na kilichomkuta, baada ya hapo akaanza kufundishwa kutumia kompyuta akiwa na hali yake ya kutoona.

"Katika kituo hiki mafunzo hayo yanatolewa na wasioona wenzao ambao wamefuzu vyema mafunzo na wanauelewa mzuri wa matumizi ya teknolojia hiyo," anasema, akijivuna alielewa vizuri na ana bidii kujifunza, hata akamudu kutumia kompyuta masomoni.

Dk. Kisanga anaeleza UDSM wapo makini katika kuhudumia wenye mahitaji maalum kulingana na uhitaji, wanahakikisha anakuwa salama na watu wa kumsaidia kwenye shughuli zake.

Ni watu anaowataja wameandaliwa mazingira mzuri ya kwenda masomoni, kuna bajaji maalum wamepewa namba za madereva, kwa kuwa chuo ni kikubwa wanatumia usafiri. Pia, wanatumia wanapokuwa kwenye mafunzo ya vitendo.



Rukia Mohamed, akitumia simu yake **PICHA: BEATRICE MOSES.**

"UDSM imeanza kudahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu mwaka 1978 na walikuwa wanafunzi wasioona wawili. Mpaka sasa wanafunzi waliodahiliwa wasioona 275, waliomaliza 210 na wanaoendelea na masomo ni 65," anasema.

Hadi sasa idadi ya wenye mahitaji malum wanaopokewa UDSM, imekuwa ikiongezeka wanafunzi mfano wanafunzi wasioona walijisajili kwenye masomo kwa mwaka 2022/2023 walikuwa 20, wakati 2023/2024 walikuwa 18, hatua inayoonyesha juhudi kuwawezesha wenye sifa za kusoma elimu ya juu zinazingatiwa vyema hadi kwa makundi maalum.

"Huduma ya vifaa vya teknolojia kama kompyuta kwa wanafunzi wasioona yalianza mwaka 2008, hadi sasa walionufaika ni takribani 150 ambao wana uwezo wa kutumia vifaa kama kompyuta, 'Braille Note Takers, Braille Sense na Orbit Reader 20," anazitaja meneja huyo.

Dk. Kisanga anasema kituo chao kinakabiliwa na changamoto, baadhi ni wanafunzi wanaotumia 'nukta nundu' kutokana na mazoea, wanakwepa kujifunza kutumia kompyuta, hali inayowasababishia changamoto kwenye ajira, kwa kuwa lugha hiyo haitumiki kwenye ofisi nyingi.

Pia, anasema waajiri wengi wanakwepa kuwaajiri wenye ulemavu kutokana na dhana ya unyanyapaa, ingawaje wahitimu wao UDSM wanakuwa na sifa za kufanya kazi -wameiva kama walivyo wahitimu wengine wa kawaida.

Ikirejewa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inahimzia fursa usawa katika utoaji elimu na mafunzo ni muhimu kwa kila Mtanzania kupate fursa hiyo.

Inahimizwa ushiriki wa jinsia zote katika elimu na mafunzo, kuhakikisha kila Mtanzania anashiriki kuchangia maendeleo hayo na kuzingatia umuhimu huo, serikali imeendelea kutoa elimu na mafunzo kwa kuzingatia usawa kwa makundi yote pasipo kumwacha yeyote nyuma.

Vilevile, serikali imekuwa ikishirikiana na wadau wa elimu, kupanua na kuboresha mazingira ya utoaji elimu jumuishi na kumwezesha kila Mtanzania kupata fursa hiyo katika hali halisi ya yanavyopatikanaji rasilimali nchini.

AFYA

# Wana- Kanda ya Ziwa wanavyohama toka uzazi foleni hadi kuacha nafasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA



Wazazi wakiwa katika wodi hospitalini mikoa ya Kanda ya Ziwa. **PICHA: MTANDAO**

UZAZI wa kuacha nafasi umeonyesha kichocheo cha ukuzaji uchumi kifamilia, kutokana na wazazi kupata muda kufanya shughuli za maendeleo, wakipanga bajeti zao kwa usahihi na wanaowahudumia watoto kukikidhi mahitaji yao.

Ni aina ya uzazi unaoruhusu usimamizi bora wa fedha na kuongeza uwezekano wa matumizi ya busara ya rasilimali na wazazi kupata muda wa kufanya shughuli zao kiuchumi.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), linasema uzazi wa kuacha nafasi ni muhimu kwa maendeleo endelevu na mapambano ya umaskini katika kaya.

Muuguzi wa Uzazi wa Mpango na Upimaji Saratani, kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa Shinyanga, Maria Barikwingenza, anasema uzazi wa kuacha nafasi kwa mwanamke unaimarisha afya yake na atakuwa na nafasi ya kufanya shughuli zake kiuchumi, akiinua kipato cha familia.Anaeleza, hata baba anapata nafasi nzuri ya kuhudumia familia kwa kupanga bajeti zake kwa usahihi na kufanya maendeleo katika kaya yake.

"Uzazi wa kuacha nafasi ni muhimu sana katika familia, kwa sababu ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa maendeleo, kutokana na kupanga bajeti zao vizuri pamoja na kuwa na muda mwingi wa kufanya shughuli za kiuchumi," anasema Maria.

Anafafanua mwitikio wa wanawake kujitokea, kupata huduma ya uzazi kudhibiti uzazi mfululizo watoto katika hospitali hiyo siyo mkubwa.

Maria anasema, wao wataalamu wamekuwa wakijitahidi kutoa elimu kwa wajawazito wanaofika kujifungua hospitalini hapo.

"Huduma za kudhibiti uzazi zinatolewa bure, na wanawake ambao tunawapatia huduma hizi. Kwanza, huwa tunawapatia ushauri na wengi huwa wanapenda kutumia njia ya vidonge, sindano pamoja na njiti na kwa mwezi mmoja huwa tunawapatia huduma wanawake 10," anasema Maria.

### UTAFITI ULIVYO

Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Viashiria vya Malaria Tanzania (TDHS) 2022, vinawarejea wanawake wanaotumia njia za kudhibiti uzazi kwa walioolewa ni asilimia 38, ambao hawajaolewa wako asilimia 45.

Utafiti huo unautaja mkoa wa Shinyanga, ni asilimia 35 tu ya wanawake wanaotumia njia za kudhibiti uzazi.

Mratibu wa Elimu Afya kwa Umma Mkoa wa Shinyanga, Moses Mwita, anasema kutokana na mwitikio huo kuwa mdogo wa wanawake kutumia njia za uzazi, wamekuwa wakiwapa elimu wanawake kupitia vyombo vya habari, majukwaa mbalimbali na mikusanyiko.

Anasema elimu hiyo wamekuwa wakiitoa kila mwezi, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, likiwamo shirika binafsi.

Hapo wamekiwa wakiacha nafasi katika uzazi, huku wakiona faida kubwa kwa afya ya mama na mtoto, inayobaki kichocheo cha ukuaji uchumi nchini.

"Hapa Shinyanga tuna wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 2,800 ambao hutembelea kila kaya na kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa wanawake na uzazi wa mpango," anasema Mwita.

Hadi sasa mkoani humo, kuna mradi uitwao 'Maamuzi Yako Kesho Yako' ulioko katika ngazi awamu ya nne, ulioanza Januari mwaka huu na unatarajiwa kudumu hadi Desemba 2026, ukilenga elimu ya uzazi wa kuacha nafasi katika familia.

Mratibu wa Mradi huo, Godbless Mtega, kutoka shirika binafsi mkoani humo, anasema wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na serikali, wakipanga ratiba ya kutoa elimu na huduma ya uzazi wa kuacha nafasi.

"Mradi huu wa 'Uamuzi Wako Kesho Yako' ni huduma jumuishi, ambayo timu ya wataalamu wa huduma za uzazi huambatana na wataalamu wa chanjo kwenda kwenye kijiji chenye ratiba ya huduma hizo, ambao hutolewa elimu na ushauri kuhusu uzazi wa kuacha nafasi," anasema Mtega.

Anataja takwimu kwa kipindi cha kuanzia Januari 2024 hadi Septemba mwaka huu, kuwa timu ya wataalamu wa afya ya uzazi wakishirikiana na watoa huduma kutoka vituo vya serikali, wamefikia wanawake 5,222 wakiwapatia njia za uzazi za kisasa, walizochagua kwa hiari yao baada ya kupewa elimu na ushauri.

Mtega anaongeza kuwa, wamekuwa wakiwajengea uwezo watoa huduma katika hospitali, vituo vya afya, zahanati na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ili kuwaongezea ujuzi wa masuala ya uzazi huo.

"Uzazi wa kuacha nafasi ukifuatwa vyema ngazi ya kaya, familia zitakuwa na uchumi imara, sababu watapangilia bajeti zao vizuri, na hata taifa pia litakuwa kiuchumi sababu halitakuwa na idadi ya watu wengi wasio na kazi," anaongeza.

Mhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, Getruda Emmanuel, anasema wamekuwa wakitoa elimu kwa wanawake kuhusu umuhimu wa kuzaa kwa kuacha nafasi, kupitia mikutano mbalimbali na hata kutembelea kila kaya.

Anasema wanawake wa vijijini, wengi hawana elimu ya afya ya uzazi, hivyo wao wahudumu wa afya ngazi ya jamii, hulazimika kuwatembelea katika ngazi ya kaya kuwaelimisha na kuwaelezea faida ya kuzaa kwa kuacha nafasi.

### WANUFAIKA WANENA

Mama Lishe, Rejina Malongo, anasema ametumia njia za kudhibiti uzazi tangu mwaka 2001 na zimemsaidia kupata muda wa kufanya shughuli zake za kiuchumi.

Anasema, hadi sasa ana watoto watano, wote amewapata akiacha nafasi kwa miaka miwili hadi mitatu, inampata muda wa kutosha kufanya shughuli zake za mama lishe.

"Mwanamke akizaa kwa kuacha nafasi, kwanza atakuwa na afya njema pamoja na watoto wake kama unavyoniona mimi, pia atapata muda mwingi wa kufanya shughuli zake za kiuchumi," anasema Rejina.

Mwingine, Rehema Matondo, mkazi wa wilayani Shinyanga, anasema vijijini, wanawake wengi hawana elimu ya afya ya uzazi, na ndiyo maana huzaa watoto mfululizo bila ya kuacha nafasi na mara nyingi wanakuwa tegemezi kwa waume zao, sababu hawana muda wa kufanya shughuli zao kiuchumi.

Anashauri, elimu hiyo ya afya ya uzazi inapaswa itolewe sana vijijini kwa wanawake na waume zao, kwa sababu wanawake wa vijijini hawana uamuzi katika uzazi, bali hutawaliwa na mwanaume na kupata watoto mfululizo bila hata ya kujali afya ya mama.

Jidayi Magembe, aliyepata elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpangilio, anasema amekuwa akijifungua kwa kuacha nafasi ya miaka mitano na anapanga bajeti vizuri za matumizi ya familia, huku akifanya shughuli zake kwa uhuru. Mwanaume, Kulwa Jishosha, anasema wao vijijini huwajui kuacha nafasi, wanazaa watoto wengi wakiamini ni nguvu kazi ya kulima shambani na ndiyo utamaduni walioukuta duniani.

Mzee wa kimila, Sonda Kabeshi, anakiri utamaduni wa kijijini ni unaegemea nguvu kazi ya uzazi wa watoto wengi, lakini anasema sasa yameshapitwa na wakati.

Anasema, watoto hao wanapokuwa watu wazima na kuhitaji kujitegemea, hujikuta hawana mali, ikwamo mashamba waliolima wazazi wao.

Mzee Kabeshi anaeleza kwamba, nihali inayowafanya watoto kuwa wategemezi hadi utu uzima na baadhi ndio wanaiojitokeza hatua ya kusuka njama kuwadhuru wazazi wao, kwa tamaa ya urithi wa mali.

"Mimi nina familia mbili moja ipo Shinyanga mjini, nyingine huku kijijini Shantimba, lakini nilizaa watoto kwa kuacha nafasi na nipo vizuri kiuchumi, na watoto wangu wengine wanashughuli zao na baadhi bado wanasoma," anasema Sonda.

Anawasihi wananaume na vijana wasiige ya zamani, kwa sababu mambo mengi yamebadilika, hata kuifanya kanuni za kale kukosa nafasi katika shughuli za kimaendeleo.



# Mabinti walioacha masomo warejea shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAFUNZI wa kike 194 mkoani hapa wamerejea shuleni kuendelea na masomo kupitia Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala (SEQUIP-AEP).

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Mayeka Mayeka alitoa takwimu hizo jana kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi yaliyofanyika viwanja vya Shule ya Msingi Hogoro wilayani humo.

Mayeke, alisema serikali imeona iwape fursa tena ya kufikia ndoto zao kielimu wanafunzi hao ambao ni miongoni mwa walioacha masomo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kupata ujauzito wakiwa shuleni.

Awataka wasichana wengine ambao kwa bahati mbaya waliachishwa masomo kwa sababu kama hizo kuchangamkia fursa hiyo ya kujiendeleza iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali wasichana ambao hawakuweza kupata elimu ya sekondari kwenye mfumo rasmi kwa sababu mbalimbali, ameamua kuwarejesha kupitia mpango wa SEQUIP-AEP."

**"Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali wasichana ambao hawakuweza kupata elimu ya sekondari kwenye mfumo rasmi kwa sababu mbalimbali, ameamua kuwarejesha ..."**

"Mkoa wa Dodoma tumefanikiwa kuwarejesha shule wanafunzi wa kike 194 kupitia programu hii na zoezi la kuendelea kuwabaini na kuwasajili linaendelea," alisema.

Ofisa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Mkoa wa Dodoma, Borase Chibura, alisema kupitia utekelezaji wa programu ya Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA), wananchi hawafundishwi Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ( KKK) na Stadi za maisha ili kuwawezesha kujikwamua kimaisha.

"Dodoma ni miongoni mwa mikoa miwili nchini inayotekeleza programu ya MUKEJA kupitia vituo viwili vilivyoko katika halmashauri mbili za Kongwa na Kondoa, hali inayoongeza fursa ya upatikanaji wa elimu kwa watu wazima," alisema.

Maadhimisho hayo kwa mwaka huu kauli mbiu yake inasema: 'Ujumuishi katika elimu bila ukomo kwa ujuzi, ustahimilivu, amani na maendeleo."



Mikanoli Maloda (72), Mkazi wa Kijiji cha Chinangali 2, Kata ya Buigiri Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, akiwaonyesha waandishi wa habari eneo la shamba lake la hekari nne na nusu pembezoni mwa Mlima wa Idunda, analodaiwa kupewa mwekezaji wa Kampuni ya Chico kutoka China kwa ajili ya machimbo ya mawe, kokoto na kifusi. Maloda, ameiomba serikali kulipwa fidia tangu mwaka 2021 bila mafanikio kutoka asimamishwe kufanya shughuli za kilimo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mawakili wa serikali wapigwa msasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (CAG) imetoa mafunzo ya upekuzi wa mikataba inayoingiwa na serikali kwa mawakili wa serikali wa mikoa nchini.

Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka Idara ya Mikataba, Ildephonce Mukandara aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo hayo jijini hapa.

Mukandara, alisema mafunzo hayo yamejumuisha mawakili wazoefu na wageni ili kuwajengea uwezo kufanya upekuzi wa mikataba hiyo na kutoa ushauri kwa serikali. Alisema baada ya mafunzo hayo, mawakili hao, watapitishwa katika vipengele muhimu vya kufanyiwa upekuzi kwenye mikataba ili kuwa na uwezo mkubwa wa kuishauri serikali.

"Mawakili wa serikali ni watu muhimu sana kuisaidia serikali kwenye mikataba, hivyo ni muhimu wakapata mafunzo ya kutekeleza wajibu wao huu wa upekuzi wa mikataba kwa ufanisi mkubwa zaidi," alisisitiza Mukandara. Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Wakili wa Serikali, Irene Msuya, alisema ni muhimu kwa kuwa yatawasaidia kwenye utendaji kazi wao.

# DC aagiza elimu dhidi ya rushwa itolewe shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ameagiza kampeni ya kupinga rushwa nchini itumike kutoa elimu kwa wanafunzi ili kutokomeza vitendo hivyo nchini.

Agizo hilo alilitoa jijini hapa jana wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Shekimweri.

"Hii kampeni ikatumike kuelimisha jamii madhara yatokanayo na rushwa kwa mtoa rushwa na mpokeaji rushwa hususani shuleni na vyuoni," alisema na kuongeza kuwa:

"Nawashukuru Mabalozi wa Sauti ya Wapinga Rushwa Tanzania (ACVF) kwa kuanzisha kampeni hiyo, hii inaonyesha jinsi gani mko pamoja na serikali kwenye mapambano dhidi ya rushwa."

Alisema serikali imejizatiti katika mapambano hayo dhidi ya rushwa jijini Dodoma kwa kuwa imekuwa ikizorotesha maendeleo na upatikanaji haki kwa jamii.

Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Sepesha Rushwa, Dk. Dinner Mbaga, alisema kampeni hiyo inafanyika kwa lengo la kupambana na rushwa.

Aliahidi wataendelea kushirikiana na wadau wa mapambano ya rushwa ili kuhakikisha wanaitokomeza nchini.

Awali, Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, Eugenius Hazinamwisho, aliwashukuru vijana wa ACVF wanavyojitoa katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo na kutaka jitihada hizo kuigwa na vijana wengine nchini.

"Tunaomba vijana wengine mjiunge kwenye vikundi vya mapambano dhidi ya rushwa, mkifanya hivyo mtaisaidia serikali katika mapambano dhidi ya rushwa," alisema Hazinamwisho.





# Ma-DC, ma-DED watumwa hamasa uchaguzi S/mitaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKUU wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri mkoani Mbeya wametakiwa kwenda kuwahamasisha wananchi vijijini na mitaani kushiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili wapatikane viongozi wenye sifa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya hadhara ya Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi ambaye anaendelea na ziara katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Akiwa katika Kata ya Iziwa jijini Mbeya, Homera alibaini kuwa wananchi hawana uelewa wa kutosha kuhusu uchaguzi huo na ndipo akatumia muda huo kutoa maagizo hayo.

Kwenye mkutano huo wananchi walionyesha kutofahamu tarehe ya kukoma kwa uongozi wa viongozi waliopo madarakani kwa sasa, tarehe ya kujiandikisha na tarehe ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Baada ya kubaini hayo, alisema uchaguzi huo ni muhimu na hivyo ni lazima viongozi wa serikali watoe elimu kwa wananchi ili kuwaongezea uelewa na washiriki kikamilifu kwenye uchaguzi huo.

**"Kuanzia sasa wakuu wa wilaya na wakurugenzi, zungukeni kwenye mitaa na vijiji vyote kwenye maeneo yenu kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mchakato mzima ...**

"Kuanzia sasa wakuu wa wilaya na wakurugenzi, zungukeni kwenye mitaa na vijiji vyote kwenye maeneo yenu kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi huu, tunataka wananchi wote washiriki kwenye uchaguzi," alisema Homera.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, alisema mchakato wa uchaguzi huo unaanza na uandikishaji wa wapigakura ambao unatarajiwa kuanza Oktoba 11 mwaka huu ambapo aliwataka wananchi wote kujitokeza kwenye vituo vilivyoainishwa ili wajiandikishe.

Alisema mtu yeyote ambaye hatakuwa amejiandikisha hataruhusiwa kushiriki uchaguzi huo na kwamba wale watakaokuwa wameandikishwa watatakiwa kupiga kura kwenye vituo walivyojiandikisha. Alisema kunabaadhi ya wananchi wanachanganya kati ya Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na hivyo wanaamini kwamba wakiwa na vitambulisho vya kupiga kura wataruhusiwa kushiriki uchaguzi huo.

Alisema Uchaguzi Mkuu unasimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi lakini Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akizungumzia jambo hilo, Prof. Kabudi alisema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndio utakaoleta picha ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani na hivyo akawataka wananchi wote kushiriki ili wapate viongozi watakaowaletea maendeleo.

Aliwataka wananchi kuwachagua viongozi waadilifu na wachapakazi na kuacha kuongozwa na mihemuko akidai kuwa wakichagua viongozi wasiokuwa waadilifu wanaweza wakawasababishia matatizo kwenye maeneo yao.

Pia, aliwataka wasimamizi wa uchaguzi huo kuwa waadilifu kwa kusimamia sheria za uchaguzi na kuheshimu viapo walivyoapa ili uchaguzi huo ufanyike kwa haki.



Baadhi ya watoto kutoka Bonde la Mwakaleli Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, wakifuatilia mkutano wa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi (hayupo pichani), alipokuwa kwenye ziara ya kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waziri aagiza udhibiti moto kwenye misitu

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, ameziagiza halmashauri nchini kuzuia mianya inayosababisha moto kwenye maeneo ya misitu, huku akisisitiza matumizi ya sheria ndogo za vijiji kwenye kuwashughulikia wanaochoma misitu.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi mbalimbali ikiwamo wa serikali katika kikao kilichofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Makete mkoani Njombe.

"Kila kikao cha serikali ya kijiji ajenda ya kudhibiti moto iwe ya kudumu na ninashauri kamati ya kudhibiti matukio ya uchomaji moto iwe mpaka kwenye ngazi ya kijiji au kata," alisema Chana.

Pia, alisisitiza kuhusu kufanya ulinzi shirikishi ili kujua waanzilishi wa moto sambamba na kufanya utafiti wa miti inayofaa kwa mkaa ili wananchi wapewe vibali vya kuipanda, waachane na uchomaji misitu.

"Naziagiza mamlaka za utafiti wa misitu TAFORI kuhakikisha kuwa wanafanya utafiti ambao zitapunguza ukataji miti ya asili kwa ajili ya mkaa, kwa kubuni miti ya kupanda ambayo itakuwa inatumika katika uchomaji mkaa," alisema Dk. Chana.

Dk. Chana alisema ni vema kukapatikana majina ya vijana katika kila kijiji wilayani humo ambako kumekuwa na uharibifu wa uchomaji moto ovyo ambao watapewa mafunzo ya ulinzi wa maliasili na utunzaji wa mazingira.

Waziri huyo aliiagiza idara ya kilimo kuhakikisha kuwa wanatoa elimu ya kutosha kuhusu namna bora ya kuandaa mashamba pamoja na madhara ya uchomaji moto ovyo.

Awali akiwasilisha taarifa ya matukio ya uchomaji moto wilayani Makete kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2024/2025, Ofisa Misitu George Africanus alisema kuwa jumla ya eneo lenye ukubwa wa ekari 1960 zimeungua kwa moto zenye thamani ya Sh. bilioni 1.4 na kusababisha hasara kwa wamiliki.

# NSSF yakusanya tril. 8/- miaka mitatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MATUMIZI ya teknolojia ya kidijitali kwenye ukusanyaji wa mapato imeuwezesha Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kukusanya zaidi ya Sh. trilioni 8.5 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 60 ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja ambayo kitaifa yanafanyika mkoani hapa.

Wadau mbalimbali walihudhuria uzinduzi wa maadhimisho hayo wakiwamo wanachama, taasisi za fedha na wadau kutoka kwenye kampuni mbalimbali za mkoa huo.

Mshomba alisema mfuko huo umewekeza zaidi kwenye matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi wake hali ambayo ndiyo imekuwa chachu ya ongezeko la ukusanyaji wa mapato.

Alisema kwa sasa nyenzo kubwa inayotumika kwenye utendaji kazi ni TEHAMA na akawahakikishia wanachama na wadau kuwa fedha zao zipo usalama kutokana na teknolojia hiyo.

"Sasa hivi dunia imebadilika, vitu vingi vinafanyika kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kwa hiyo hata sisi lazima tuendane na mabadiliko haya na ndiyo maana tuliamua kuingia huko na matokeo yanaonekana," alisema Mshomba.

Meneja wa Huduma kwa wanachama wa mfuko huo, Robert Kadege alisema mfuko huo unaendelea kuboresha mifumo ya kidijitali kwa wafanyakazi na wanachama kwa kuwajengea uwezo ili waendane na mabadiliko.

Alisema wamekuwa wakitoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyaka ili waongeze weledi wa kuwahudumia wanachama ikiwa ni pamoja na kuwafundisha matumizi ya teknolojia.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Ekwali Mujungu alisema idadi ya wanachama imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na huduma bora ambazo wamekuwa wakizitoa.

Alisema Juni 2023 mfuko huo ulikuwa na wanachama 1,189,00 lakini mpaka kufikia Juni 2024 wanachama wameongezeka na kufikia 1,342,654 na kwamba ongezeko hilo linatokana na elimu ambayo imekuwa ikitolewa kwa wafanyakazi.

## Bei ya petroli, dizeli, mafuta ya ndege yashuka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya ndege visiwani Zanzibar imepungua kipindi cha Oktoba ikilinganishwa na Septemba.

Akitangaza mwenendo wa bei ya mafuta, Ofisa Uhusiano kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Shara Chande Omar, alisema mafuta ya petroli yatauzwa kwa Sh. 3,008 kwa mwezi huu kutoka Sh. 3,164 ya mwezi uliopita.

Alisema kwa mafuta ya dizeli yatauzwa Sh. 3,111 kwa lita kutoka Sh. 3,247 ikiwa na tofauti ya shilingi 136 sawa na asilimia 4.19.

Kuhusu mafuta ya ndege alisema yatauzwa kwa shilingi 2,827 kwa mwezi huu kutoka shilingi 2,837, huku mafuta ya taa yataendelea kuuzwa kwa bei ya shilingi 3,200.

Shara alizitaja sababu za kubaki kwa bei ya mafuta ya taa kila mwezi, alisema hivi sasa mafuta hayo yanapouzwa yanapigwa lita ili yasiweze kutumika ambapo husababisha bei yake kupanda zaidi.

“Bei yake kila mwezi inapanda huko tunaponunua na itafika wakati mafuta ya taa yatakuwa hayatumiki na ndio maana tunahamasisha utumiaji wa gesi safi ya kupikia,” alisema.

Aidha, alisema pia mafuta ya taa watu wengi wanayatumia kwa kufanya udanganyifu wa kuchakachua mafuta na ndio maana bei yake haishuki ili watu wenye tabia hiyo waache.

Alisema sababu za kupungua kwa bei hizo za mafuta kwa mwezi huu, zinatokana na kushuka kwa bei za ununuzi katika soko la dunia, kushuka kwa gharama za usafirishaji pamoja na mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni kwa mwezi huu.

Hata hivyo, alisema ZURA hupanga bei hizo kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwamo wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani.

Alitaja sababu zingine ni gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar- es Salaam na Tanga, gharama za mabadiliko ya fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta, gharama za usafiri, bima na premium hadi Zanzibar, tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

# Mama Mwinyi: Miradi ya afya huimarisha huduma za afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, amesema uwajibikaji katika miradi ya afya ni moja ya mpango wa serikali katika kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano ulioandaliwa na Shule ya Liverpool of Tropical Medicine (LSTM) uliolenga uboreshaji wa huduma za maradhi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), kifua kikuu (TB) na malaria uliofanyika mjini Zanzibar.

Alisema serikali imewekeza katika masuala ya afya ili kuona wananchi wanaishi katika mazingira mazuri na afya bora hususani afya ya mama na mtoto kwa kuwa ni suala linalohitaji kushughulikiwa zaidi ikiwa ni moja ya mikakati ya serikali ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

“Afya na mama na mtoto ni jambo la kulizingatia zaidi kwani kinamama wanapata matatizo mengi wakati wakiwa na ujauzito na baada ya kujifungua,” alisema.

Hivyo alisema programu hiyo ni muhimu na itaimarisha afya ya mama na mtoto pamoja na jamii kwa ujumla, hivyo kufikia lengo la taifa na kimataifa la kupunguza vifo vya mama na watoto lakini kuimarisha afya ya msingi.

**Waziri wa Wizara ya Afya, Nassor Ahmed Mazuri, alisema awali wajawazito wengi walikuwa wanafariki na watoto chini ya miaka mitano walikuwa wakiathiriwa...**

Waziri wa Wizara ya Afya, Nassor Ahmed Mazuri, alisema awali wajawazito wengi walikuwa wanafariki na watoto chini ya miaka mitano walikuwa wakiathiriwa na malaria lakini sasa hali hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo alisema mradi huo umekuja kuwathibitishia kwamba matatizo ya TB, VVU na malaria kwa wajawazito ni suala la kushughulikiwa na kwamba wizara inafanya uwekezaji kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi.

“Bado tuna njia ndefu ya kwenda ili kupunguza vifo, hivyo tunataka ushirikiano wa wadau mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari ambapo tukifanya hivyo tunaweza kufikia malengo ya kuwa na vifo vya watoto visivyozidi 12 kwa kila kizazi hai 1,000 na mama chini ya 75 kwa 100,000,” alisema Mazrui.

Mkuu wa Idara ya Kimataifa ya Afya ya Umma wa shule hiyo, Prof. Charles Ameh alisema mradi huo unatekelezwa katika nchi za Kenya, Nigeria na Tanzania na kwamba unatoa hamasa kwa jamii kujitokeza katika vituo vya afya kujua afya zao na kupatiwa matibabu bora.

Naye Mkuu wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto unaohusiana na maradhi ya VVU, TB na malaria Zanzibar, Salma Abdi Mahmoud, alisema mbali na jitihada hizo lakini bado kuna changamoto ikiwamo kinamama kuwa na damu ndogo wakati wa kujifungua kunakosababishwa na kutohudhuria kliniki mapema.



Wananchi mbalimbali wa Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar wakijitokeza katika vituo jana, kwa ajili ya kuboresha taarifa zao na kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, uandikishaji ulioanza jana hadi Oktoba 13, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Mazrui asisitiza ushirikiano kazini ili kuongeza ufanisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema pamoja na mabadiliko yaliyoko katika sekta ya afya, watendaji wanatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuiongezea ufanisi.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya udhibiti wa viashiria hatarishi, uhujumu uchumi, sheria za utumishi wa umma na huduma kwa wateja kwa wakurugenzi na wakuu wa taasisi zilizomo ndani ya wizara hiyo.

Alisema toka mwaka 2021 alipoteuliwa kuwa waziri wa wizara hiyo ameshuhudia mabadiliko na mageuzi makubwa ya mifumo na utendaji kazi lakini bado hajaridhika.

Aidha, alisema mkutano huo ni muhimu, kwamba watapata fursa ya kujadili matatizo yanayoikabili Wizara ya Afya ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi.

Hivyo aliwataka kufanya kazi kwa ajili ya wananchi, hivyo mkutano huo uwe chachu ya kuongeza nidhamu kazini, kufuata taratibu za kazi, sheria na kanuni ambazo zitajadiliwa.

Alisema serikali inafanya kazi ya kujenga miundombinu, kuleta vifaa, dawa na vitu vingi na katika kipindi kifupi kijacho Zanzibar kutakuwa hakuna ukosefu wa miundombinu ya afya.

Naye Katibu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema malengo ya mafunzo hayo yamegusa sehemu kuu tatu ikiwemo huduma kwa wateja, sheria na kanuni za utumishi.

“Tulikuwa na changamoto za hapa na pale ikiwamo miundombinu ambapo serikali inaelekea kuimaliza, sasa hivi tunapambana na suala la huduma, ndiyo maana tukaona tulete mafunzo haya,” alisema.

Hivyo alisema baada ya mafunzo hayo yatafanyika kwa watendaji wa ngazi ya chini, lengo likiwa ni kutatua matatizo yenye kuhusiana na changamoto hizo yataweza kutatuka katika wizara yao.

Mkurugenzi Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Salim Slim, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha utendaji kazi wao ili kufikia malengo ya viongozi wa nchi.

Alisema kuna baadhi ya mambo wamefanikiwa lakini yapo mambo ambayo bado yanasuasua na kushindwa kufikia malengo.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utumishi Serikalini kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Sheria, Katiba, Utumishi na Utawala Bora, Shaibu Ali Mwezema, alisema ni vyema wafanyakazi wakazisoma sheria, kanuni na sera ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Alisema kama mfanyakazi atafanya kazi bila kufahamu vitu hivyo hawezi kufikia malengo yanayokusudiwa na serikali na dhamira ya kuwa na utumishi uliotukuka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VYETI VIMEPOTEA



**NDG. SENDAMA PETER SENDAMA,** Anatangaza kupotelewa na veti vifuatavyo :

1) Cheti cha Chuo cha Uhasibu, Arusha, chenye Index na. **MPSM-01-0064-2022** cha mwaka 2023. (PHQ/RUV/SON/4817/2022)
2) Academic Transcript, chenye Index na. **MPS-01-0064-2022, (PHQ/RUV/SON/4821/2024)**

TAARIFA ZA POLISI ZIPO KWENYE MABANO KWA YEYOTE ATAKAYEVIONA ANAOMBWA KURIPOTI KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU

## KUPOTEA KWA CHETI



**RATIFA JUMA KASSIMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0528/0037/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SABASABA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MTW/MTW/6317/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISAYA CHARLES VIYANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 909 AME.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI CONTROL NUMBER: **9910842499125**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VILLELA WAANE KEJO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T276 DKN TOYOTA IST** CHASSIS **NCP600233162** ENGINE **2NZ3870132** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**PHQ/ARU/ARU/38233/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULLAH MUHAMMAD NASSAR** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T 923 DJX** CHASISI NAMBA **WBANE32020CM75831,** ENGINE NAMBA **06576359N52325AL** ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA
**PHQ/DAR/KIN/21827/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FIDON RWEZAHULA MWOMBEKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 869 BMT** na CHASSIS NAMBA: **AE1116115200.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/38280/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**REMI CHALES GOTI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki aina ya King Lion yenye namba za usajili **MC269CLC,** Chaisis namba ***LZL15P900KHL52821*** na Engine namba **KL162FMJ*191152821*** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/MAN/BAB/8617/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 24876 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PAUL TUMSIFU SOMI**

**And**

**IN THE MATTER OF PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY TUMAINI KWEKA also known as TUMAINI PAUL SOMI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 06 Day of 11...................... 2024

Dated at Dodoma this 02nd Day of OCTOBER 2024

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 23604 OF 2024**

**In the Matter of the late JOSEPH JOSEPH MUSHI**

**And**

**In the Matter on an Application for letters of administration by ROSE JOSEPH MUSHI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 31 day of 10...................... 2024
Presented for filling this 3 Day of 10................2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**

**SHAURI LA ARDHINA. 18825/2024**

**RAMADHANI SANYA ..............................MLETA RUFAA**

**BI. ELIZABETH SUBETH............................MJIBU RUFAA**

**KWA: BI. ELIZABETH SUBETH**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA.18825/2024**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma. mbele ya Mhe. Jaji I. D. MUSOKWA wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu kamili (9:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 5/11/2024.
**HIVYO BASI;** Unatakiwa Ufike wewe wenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .
**NA ENDAPO;** Hutofika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi wa Oktoba, 2024..

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) ARUSHA**
**MAHALI ARUSHA**

**MAOMBI NA.68 YA 2024**
**UTEKELEZAJI WA HUKUMU**

**KISAKA INNOCENT MBAGA.......................MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**AYUB ELIAS MAKOLO...........................MSHINDWA TUZO**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

**KWA: AYUB ELIAS MAKOLO......................POPOTE ULIPO**

**KISAKA INNOCENT MBAGA** amefungua shauri la utekelezaji wa hukumu mbele ya Baraza la ardhi na Nyumba wilaya ya Arusha. Shauri husika limepangwa kutajwa mbele ya Mh. G. Kagaruki, Mwenyekiti tarehe 22/10/2024. Saa tatu kamili asubuhi. Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria siku hiyo wewe au wakili wako au mtu yeyote utakayempa maelekezo juu ya shauri hili. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa dhidi yako pasipo wewe kusikilizwa. Nakala ya maombi haya inapatikana katika Ofisi za Baraza zilizopo katika jingo la mkuu wa wilaya Arusha.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wngu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 23 mwezi Septemba, mwaka 2024

MWENYEKITI

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**

**EXECUTION NO 20572 OF 2024**

**TATA AFRICA HOLDING TANZANIA LTD............D.HOLDER**

**VERSUS**

**HAMADI ABDALLAH KANAMA..........................J.DEBTOR**

**NOTICE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for MENTION in the Resident Magistrate court of Moshi at Moshi on 10th day of OCTOBER, 2024 at 09:00 am before Honourable A.A. MKAMA – PRMA
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Mwananchi newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the court this 3rd Day of SEPTEMBER, 2024

RESIDENT MAGISTRATE
MOSHI
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MOSHI

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARIKIMATAIFA



Mwanajeshi wa Israel akilinda mpaka wa nchi yake na Lebanon. **PICHA : ALLIANCE**

## WIKI MOJA NGUMU

# Gachagua sasa kuisubiri Seneti

**NAIROBI, Kenya**

NI dhahiri Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, amebakisha wiki moja ngumu na yenye mashaka ili kubaki madarakani baada ya kutumikia kwa muda wa miaka miwili.

Usiku wa kuamkia jana, wabunge wa nchi hiyo walipiga kura ya kihistoria ya kumwondoa madarakani Gachagua kutokana na tuhuma za ufisadi, kutumia vibaya madaraka na kuligawanya taifa kwa ukabila.

Jana, Bunge la Seneti nchini humo lilipokea rasmi uamuzi wa bunge la kitaifa na hivyo litachukua muda wa wiki moja kabla ya wajumbe kuanza kujadili hoja ya kumwondoa madarakani Gachagua, siku ya Jumatano na Alhamisi wiki ijayo.

Bunge hilo la Seneti jana lilikutana kupokea hoja hiyo kutoka kwa kiongozi wa wajumbe wenye idadi kubwa, Aaron Cheruyot, mara baada ya bunge la kitaifa kupiga kura ya kumwondoa madarakani Makamu wa Rais.

Katika mchakato huo, Bunge la Seneti litakaa kama mahakama kwa kuchunguza mashtaka anayokabiliwa nayo Gachagua na kusikiliza tena ushahidi kutoka pande zote zinazohasimiana.

Katika zoezi la upigaji kura, wabunge wamepitisha hoja ya kumwondoa madarakani Naibu wa Rais Gachagua, kwa kura 281, huku wabunge 44 wakipinga.

Kabla ya wabunge kupiga kura, Rigathi Gachagua alikwenda mbele ya bunge na kuwasilisha utetezi wake kuusu tuhuma 11 anazokabiliana nazo na kueleza zote hazina ukweli.


Katika utetezi wake, Gachagua alieleza kwamba yeye amekuwa mbuzi wa kafara na kwamba hana hatia.

Alisema siku zote anafanya kazi kubwa ya kutetea maslahi ya Wakenya.

Siku moja kabla ya kufika bungeni, kiongozi huyo aliwaambia waandishi wa habari kwamba hatajiuzulu wadhifa wake na yuko tayari kupambana hadi tone la mwisho.

Tofauti kati ya Naibu huyo wa Rais na Rais William Ruto, zimeongezeka kiasi cha viongozi hao kukatisha mawasiliano na kupeana maneno makali.

Gachagua awali alikuwa na matumaini hoja hiyo haiwezi kupelekwa bungeni bila idhini ya Rais Ruto, na alipowasilishwa



Rigathi Gachagua.

ilionekana wazi kwamba kiongozi huyo ameidhinisha.

**Nini kilifanyika?**

Baada ya hoja hiyo kuwasilishwa bungeni, wabunge walijadili mmoja mmoja na hatimaye alipewa nafasi Gachagua kufika mbele ya chombo hicho kujitetea.

Baada ya kumaliza utetezi wake, wabunge walipiga kura ya kumwondoa madarakani makamu huyo wa rais.

Awali, Gachagua alipinga tuhuma hizo zilitajwa ndani ya bunge kuanzia ile ya umiliki wa kiasi kikubwa cha mali ambayo alidai ilikuwa ni urithi kutoka kwa marehemu kaka yake gavana wa zamani wa Nyeri, Nderitu Gachagua.

Alidai kuwa madai hayo ni njama ya kisiasa inayoendeshwa na watu wenye hila, wasioogopa kuanzisha vita na wafu ili kujikita uongozini.

**Hatua itakayofuata**

Spika wa Bunge, Moses Wetangula, ana siku mbili za kumpa taarifa Spika wa Seneti kuhusu matokeo ya mchakato wa kura.

Kisha, Spika wa Seneti Amason Kingi ana siku saba kuwafahamisha maseneta kwa ajili ya kuanza kikao cha upitiaji wa hoja hiyo moja.

Baada ya hapo, Seneti ina siku zingine kumi za kuwasilisha kesi ndani ya bunge.

Huenda kikao cha Bunge la Seneti kitaanza Jumanne Oktoba 22, mwaka huu.

Hoja hiyo ya kumwondoa madarakani Gachagua inaweza kusikilizwa katika kikao cha pamoja au kijiunda kama kamati, lakini kutokana na uzito wake, huenda kikawa kikao cha seneti nzima.

Spika wa seneti ataongoza kesi hiyo, maseneta watapata nafasi ya kumhoji Gachagua huku mawakili wake wakitarajiwa kuwahoji mashahidi waliowasilishwa na bunge.

Mmoja wa mashahidi hao ni Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja.

Baada ya mashtaka kusikilizwa katika Bunge la Seneti, wajumbe watapiga kura, endapo theluthi mbili watakubali Naibu Rais atakuwa ameondolewa rasmi madarakani.

Mchakato huo ni kulingana na utaratibu wa kumwondoa madarakani ulioainishwa chini ya Kifungu cha 150 cha katiba.

Hata hivyo, Naibu wa Rais atasalia madarakani iwapo hoja hiyo itakataliwa na theluthi moja ya wajumbe, au iwapo Seneti itaunda kamati ambayo itapata sababu za mashtaka kutokuwa na msingi ithibati.

Naibu Rais pia atakuwa na haki ya kufika au kuwakilishwa mbele ya kamati maalum wakati wa uchunguzi dhidi yake.

Kamati Maalum inaweza kusikiliza hoja za mwakilishi au mbunge aliyewasilisha hoja hiyo kutoka Bunge la kitaifa na wajumbe wengine.

Ikiwa kamati maalum itaripoti kwamba maelezo ya tuhuma yoyote dhidi ya Naibu Rais hayajathibitishwa, mashauri mengine hayatachukuliwa chini ya Ibara ya 145 ya Katiba kuhusiana na madai hayo.

Iwapo yatathibitishwa, bunge la Seneti, baada ya Naibu Rais kupata nafasi ya kusikilizwa, litapiga kura kuhusu mashtaka dhidi yake.

Seneti itapiga kura ya ‚ndiyo' au ‚hapana' kwa kila shtaka dhidi yake.

Iwapo angalau theluthi mbili ya wajumbe wote wa Seneti watapiga kura kuunga mkono shtaka lolote la kumshtaki, atalazimika kuachia nafasi yake.

Ikiwa chombo hicho hakitathibitisha, Naibu wa Rais ataendelea kushikilia wadhifa wake.

***BBC***

## EU yaiunga mkono Morocco dhidi ya uamuzi wa ECJ

**RABAT, Morocco**

NCHI zaidi zimejiunga katika orodha ya nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) zinazopinga uamuzi wa upendeleo wa Mahakama ya Ulaya (ECJ) unaolenga makubaliano ya ushirikiano kati ya umoja huo na Morocco.

Jumamosi iliyopita, Ureno ilisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya EU na Morocco katika nyanja ya biashara ya uvuvi na kilimo ni muhimu.

Katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ureno, ilisema ina nia ya kufanya kazi na washirika wa Ulaya ili kuimarisha ushirikiano huo katika nyanja zote.

"Ureno inachukulia ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na Morocco kuwa ni muhimu na itafanya kazi na washirika wa Ulaya na taasisi za Umoja wa Ulaya kuimarisha ushirikiano huo katika nyanja zote," ilisema wizara hiyo.

Taarifa hiyo ilisema nchi hizo mbili zinadumisha ushirikiano wa kimkakati unaosimamiwa na uhusiano wa muda mrefu wa heshima na urafiki uliojaa umuhimu wa kisiasa, kidiplomasia, na kiuchumi.

Nchi zingine za Ulaya Uholanzi, Ubelgiji, Ufaransa, na Finland pia zimepinga uamuzi huo.

Uholanzi ilisema kuwa imejikita katika ushirikiano wake wa kimkakati kati ya EU na Morocco.

"Tunarudia dhamira yetu thabiti kwa ushirikiano wa kimkakati kati ya EU na Morocco," ilisema Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi.

Ijumaa iliyopita, mahakama hiyo ilitoa uamuzi unaounga mkono Polisario na kampeni zake.

Mahakama ya ECJ iliamua kuwa Tume ya EU ilivunja haki ya kujitawala ya watu wa Sahara Magharibi kwa kufanya makubaliano ya kibiashara na Morocco ambayo yalijumuisha bidhaa kutoka majimbo ya kusini mwa Morocco.

Hata hivyo, Morocco ilijibu uamuzi huo ikieleza iko thabiti katika msimamo wake kwamba haitakubali makubaliano au nyaraka yoyote ya kisheria ambayo haiheshimu mipaka yake.

**"Tunarudia dhamira yetu thabiti kwa ushirikiano wa kimkakati kati ya EU na Morocco," ilisema Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi.**

# Zimamoto yafurahia sare Ligi ya Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kutoka suluhu, Kocha Mkuu wa Zimamoto SC, Mohamed Hilali, amewapongeza wachezaji wake kwa kuwadhibiti Maafande wenzao wa JKU na kusema kikosi chake kinarejesha matumaini ya kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Matokeo hayo yanaifanya Zimamoto ifikishe pointi tano na kukaa katika nafasi ya 10 kwenye msimamo huku JKU ikirejea kileleni baada ya kufikisha alama 10 kibindoni sawa na Mafunzo, KMKM na Uhamiaji FC.

Hilali alisema wamecheza na moja ya timu ngumu katika ligi hiyo na kitendo cha kutoruhusu kufungwa ni ishara nzuri vijana wake wameimarika.

Kocha huyo alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kwa pande zote kutokana na matokeo yaliyopatikana katika michezo yao iliyopita.

Alisema kwa upande wao walihitaji kupata pointi tatu baada ya kutoka sare mchezo uliopita wakati wapinzani wao JKU wao walifungwa.

"Mchezo ulikuwa mgumu kwa kila upande, mipango yetu ilifanana sote tulihitaji kupata point tatu lakini tumegawana alama," Hilali alisema.

Kocha huyo amewapongeza wachezaji wake licha ya mchezo kuwa na ushindani wakati wote kwa kucheza bila kuchoka dakika zote 90.

Katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, kila timu ilicheza vyema lakini golikipa namba moja wa Zimamoto, Yusuf Said, alionekana kuwa nyota wa mchezo kwa kitendo chake cha kuzuia mashambulizi yote yaliyoelekezwa katika lango lake.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata nafasi ya kukiwakilisha kisiwa hicho katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati michuano ya Kombe la ZFF hutoa mwakilishi wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# RWANDA YAIHOFIA TANZANIA MICHUANO YA CECAFA U-20

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya vijana wa umri chini ya miaka 20 ya Rwanda, Eric Nshimiyimana, amesema mechi yao ya mwisho dhidi ya Tanzania (Ngorongoro Heroes), itakuwa ngumu kwa sababu mchezo huo utaamua timu itakayosonga mbele katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), yanayoendelea nchini.

Rwanda ilifungwa bao 1-0 na Sudan katika mechi ya Kundi B iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni.

Nshimiyimana alisema mechi hiyo dhidi ya wenyeji itakuwa na ushindani kutokana na kila upande unahitaji kusonga mbele ili kupata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Afrika za U-20 zitakazofanyika baadaye mwakani.

"Mashindano haya ni magumu na yana ushindani mkubwa, kila timu imejiandaa kupata ushindi ili kusonga mbele, leo (juzi), tumepoteza mechi lakini bado tuna nafasi ya kufikia malengo, ingawa tunaenda kukutana na wenyeji Tanzania, wako nyumbani, haitakuwa mechi rahisi katika upande wetu," alisema Nshimiyimana.

Kocha huyo aliongeza anarudi kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu na anaamini watarejea wakiwa imara na wenye ,kiu' ya kupata ushindi.

"Hatujakata tamaa, lakini Tanzania wasitarajie mteremko katika mechi hiyo ya mwisho," alisema kiungo huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Rwanda (Amavubi) na APR.

Tanzania itaikaribisha Rwanda katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Mashindano hayo yanatarajiwa kuendelea leo kwa Rwanda kuivaa Kenya kwenye Uwanja wa KMC Complex kuanzia saa 10:00 jioni huku Tanzania ikiikaribisha Sudan kwenye Uwanja wa Azam Complex kuanzia saa 12:00 jioni.

Timu mbili zitakazofanya vizuri zitatinga hatua ya nusu fainali itakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu wakati fainali ikipangwa kufanyika siku mbili baadaye kwenye Uwanja wa KMC Complex.

Mashindano hayo yanafanyika ili kupata wawakilishi wawili wa CECAFA watakaokwenda kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika AFCON U-20 ambayo yatafanyika baadaye mwakani.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), wakishangilia kwa kupiga magoti baada ya kupata bao la tano dhidi ya Djibouti katika mechi ya Kundi A (CECAFA U-20), iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Ngorongoro Heroes ilishinda mabao 7-0. **PICHA: TFF**

# Azam FC yaipigia hesabu Prisons

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha Kalenda ya Kimataifa, kikosi cha Azam FC kimeanza upya mazoezi kwa ajili ya mechi yao dhidi ya Prisons itakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

Azam FC itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya wenyeji Namungo FC kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, aliliambia gazeti hili jana wachezaji wao ambao hawako katika timu za taifa wameanza kujinoa kuelekea mchezo huo ambao wanafahamu utakuwa na ushindani wakati wote.

**Ibwe alisema wanafahamu Prisons ni timu ngumu, hivyo wanahitaji kujiimarisha kwa ajili ya kuwakabili na wanaamini watavuna pointi tatu ugenini.**

"Tumeanza kuzifuata pointi za ugenini, ninaamini kama tulivyofanya kule Ruangwa, basi tutaendelea na kasi ile ile tutakapotua Sokoine, ingawa tunajua mechi haitakuwa rahisi, tunafahamiana vyema," Ibwe alisema.

Aliongeza wanashukuru wachezaji wao wako katika hali nzuri na kila mmoja anaonyesha ushindani wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

„Bado ni mapema na ligi sasa ndio imeanza kuchanganya, tumedhamiria kufanya mazuri zaidi msimu huu, hatutaki mchezo, tunahitaji kuvuna pointi nyingi zaidi kuliko msimu uliotangulia, malengo yetu ni kupata tena nafasi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema kiongozi huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WAARABU WAMTAKA BRUYNE

KLABU ya Saudia Al-Nassr ina matumaini ya kumsajili kiungo wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Team Talk)***

### TRENT KUMFUATA BELLINGHAM

MLINZI wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, anaweza kushawishika kumaliza mkataba wake Anfield ili kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bure na kuungana na mchezaji mwenzake wa England, Jude Bellingham. ***(Sun)***

### SEMENYO AGOMBEWA EPL

MSHAMBULIAJI wa Bournemouth, Antoine Semenyo, mwenye umri wa miaka 24, anawaniwa na klabu za Liverpool, Newcastle United na Tottenham Hotspur baada ya mchezaji huyo raia wa Ghana kuanza vyema msimu huu. ***(Give Me Sport)***

### LIVERPOOL, TRENT KUTETA

REAL Madrid wameimarisha mpango wa kumnunua Alexander-Arnold lakini Liverpool wanatumaini wanaweza kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kusalia katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### MARMOUSH KUMRITHI SALAH

LIVERPOOL wamemtambua mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, ambaye ni raia wa Misri, Omar Marmoush, mwenye umri wa miaka 25, na mshambuliaji wa Borussia Dortmund wa Ujerumani, Karim Adeyemi (22), kama mbadala wa winga wa Mohamed Salah (32). ***(Sky Germany)***

### RIOS ATAJWA UNITED

MATUMAINI ya Manchester United ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Colombia, Richard Rios yameimarika, huku Palmeiras ikiwa tayari kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kwa euro milioni 20 ifikapo Januari. ***(Caught Offside)***

### UNITED, ARSENAL VITANI

KLABU za Arsenal na Manchester United zinamfuatilia mlinda mlango wa Wigan Athletic, Sam Tickle mwenye umri wa miaka 22. ***(Team Talk)***

### RUSSEL MARTIN KUJADILIWA

UONGOZI wa Southampton unatazamiwa kukutana ili kujadili mustakabali wa Kocha, Russell Martin, kuhusu hatima yake ndani ya klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### MUANI KUONDOKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 25, anaweza kuhama klabu hiyo Januari lakini mabingwa hao wa Ligue 1 wanataka kumuuza kwa angalau euro milioni 70. ***(AS)***

### WIRTZ AITAMANI BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 21, ameonyesha nia ya kujiunga na Bayern Munich msimu ujao. ***(Sky Germany)***

### DAVID ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United wanaendelea kumfuatilia mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 24, kwa lengo la uhamisho ifikapo dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***



# KLOP AULA RED BULL

## ●●●Mabosi wake wapya wajivunia kumnasa mkongwe huyo...

**DORTMUND, Ujerumani**

KOCHA wa zamani wa Liverpool, Jürgen Klopp, ametia saini mkataba wa kuwa mkuu wa soka duniani wa Red Bull kuanzia Januari, mwakani.

Klopp mwenye umri wa miaka 57, aliondoka katika klabu hiyo ya Merseyside mwishoni mwa msimu wa 2023-24 baada ya kudumu kwa takriban miaka tisa, akisema anaishiwa na nguvu.“

“Baada ya takriban miaka 25 kujihusisha uwanjani sikuweza kufurahishwa zaidi kuendelea na mradi kama huu,“ alisema Klopp katika taarifa yake.

“Jukumu linaweza kuwa limebadilika lakini mapenzi yangu kwa mpira wa miguu na watu wanaofanya mchezo kama ulivyo haijabadilika.“

Red Bull inamiliki klabu kadhaa za soka duniani kote, maarufu zaidi zikiwa ni RB Leipzig inayoshiriki Bundesliga ya Ujerumani, RB Salzburg katika Bundesliga (Austria) na New York Red Bulls iliyoko Marekani. Oliver Mintzlaff, Mtendaji Mkuu wa Red Bull wa Miradi ya Ushirika na Uwekezaji, alisema ni hatua muhimu zaidi katika ujio wake katika mchezo huo.

„Tunajivunia sana usajili huu bora na wa nguvu zaidi katika historia ya soka ya Red Bull,“ alisema.

“Jürgen Klopp ni mmoja wa watu mashuhuri na wenye ushawishi mkubwa katika soka la dunia, mwenye ujuzi wa ajabu. Katika jukumu lake kama Mkuu wa soka, atakuwa mtu wa kubadilisha mchezo kwa ushiriki wetu katika soka la kimataifa na maendeleo yake.

„Tunatumaini na msukumo muhimu na madhubuti katika maeneo muhimu ili kufanya klabu kuwa bora zaidi, kwa pamoja na kibinafsi.“

Klopp alijiunga na Liverpool Oktoba, mwaka 2015 na kuwaongoza kurejea kwenye kilele cha soka la England na Ulaya.

Chini ya usimamizi wake, Liverpool walishinda taji lao la kwanza la ligi baada ya miaka 30 mnamo mwaka, 2020, taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mnamo 2019, Kombe la FA (2022) na Kombe la Carabao.





# ALISSON NJE YA DIMBA WIKI SITA

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL watakuwa bila mlinda mlango chaguo la kwanza Alisson kwa wiki sita.

Hiyo ni baada ya kuumia msuli wa paja katika ushindi wao bao 1-0 dhidi ya Crystal Palace katika mchezo wa Ligi Kuu England, uliochezwa Jumamosi iliyopita, klabu hiyo ilithibitisha jana.

Alisson mwenye umri wa miaka 32, alilazimika kutolewa nje dakika ya 79 ya mechi, na nafasi yake kuchukuliwa na kipa chaguo la tatu, Vitezslav Jaros.

Habari hizi zitakuja kama pigo chungu kwa Liverpool ambao wanakabiliwa na msururu wa mechi baada ya mapumziko ya kimataifa.

Hii ina maana Allison atakosa mechi zote za Oktoba na atatarajiwa kurudi dimbani mapema Novemba.

# Messi, Madrid wafunguka Iniesta akistaafu kimataifa

**BUENOS ARIES, Argentina**

LIONEL Messi ametoa pongezi kwa mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Andres Iniesta, ambaye amethibitisha kustaafu soka la kulipwa.

Iniesta ameachana soka akiwa na umri wa miaka 40 akicheza kwa miaka mitano nchini Japan akiwa na Vissel Kobe kabla ya kucheza msimu mmoja wa mwisho Falme za Kiarabu akiwa na Klabu ya Emirates.

Mhispania huyo alifunga bao lililoamua ushinda kwa taifa lake kwenye Kombe la Dunia la 2010.

Na aliichezea Barca mechi 674 akiwa na La Blaugrana hao kabla ya kuondoka mwaka 2018.

Alikuwa na wenzake wengi mashuhuri Camp Nou lakini bila shaka hakuna zaidi ya Messi. Wawili hao walicheza pamoja katika mechi 488 rasmi na kushinda mataji yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na tisa ya LaLiga.

Akitumia mitandao ya kijamii, Messi alimmwagia sifa kiungo huyo wa zamani, akimtaja kama mmoja wa wachezaji wake kipenzi kuwahi kushiriki naye uwanjani.

Aliandika: "Mmoja wa wachezaji wenzangu wenye uchawi mwingi na niliyefurahia kucheza nae pamoja Andres, mpira utakukosa na sisi sote. Nakutakia kila la kheri."

Wakati Barca wakimpongeza Iniesta baada ya kutangazwa kustaafu, pia alisifiwa na wapinzani wao Real Madrid, ambao walitoa heshima zao kwa mshindi huyo mara mbili wa Ubingwa wa Ulaya.

Taarifa ya Real Madrid ilisomeka: "Kufuatia tangazo la Andres Iniesta anastaafu soka la kulipwa, Real Madrid, Rais na Bodi ya Wakurugenzi wangependa kueleza kumtambua, kumstaajabisha na kumpenda mmoja wa nguli wakubwa wa soka la Hispania na dunia.

"Andres Iniesta ameboresha mchezo kupitia soka lake na maadili yake, pamoja na mataji mengi aliyoshinda wakati wa uchezaji wake. Bao lake la kipekee katika Fainali ya Kombe la Dunia 2010 nchini Afrika Kusini litabaki milele kwenye kumbukumbu ya kila shabiki wa Hispania.

"Real Madrid ingependa kumtakia yeye na familia yake mafanikio mema katika sura hii mpya ya maisha yake."

# Chelsea, Forest matatani

**LONDON, England**

CHELSEA na Nottingham Forest zimeshtakiwa na Chama cha Soka cha England (FA), baada ya wachezaji wake kufanya vurugu wakati wa sare ya 1-1 katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa Jumapili iliyopita.

Neco Williams wa Forest alizua vurugu uwanjani baada ya kumng'ang'ania Marc Cucurella wa Chelsea na kumpeleka beki wa pembeni kwenye eneo la ufundi, akimsimamisha Kocha wake Enzo Maresca.

Wachezaji kadhaa kisha walirundikana kwenye vurugu, wakiwamo wengine kutoka kwenye benchi, wakisukumana na kurushiana maneno kabla ya mwamuzi Chris Kavanagh kurejesha udhibiti.

Mechi hiyo ilishuhudia kadi 11 za njano zikitolewa kwa jumla.

"Inadaiwa klabu zote mbili zilishindwa kuhakikisha wachezaji wao hawaendi kwa njia isiyofaa," ilisema taarifa ya FA.

Klabu zote mbili zimepewa muda hadi Alhamisi (leo) kutoa majibu yao.

HABARI MICHEZO

# MAGOLI 91 YAFUNGWA LIGI BARA, FOUNTAIN YANG'ARA

Na Adam Fungamwango

HUKU raundi ya saba ikiwa imeanza, jumla ya mabao 91 yamefungwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la Nipashe, mabao hayo yamefungwa katika michezo 50 ambayo imechezwa mpaka sasa wakati ligi hiyo imesimama kupisha michezo ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025).

Mabao hayo yamefungwa na idadi ya wachezaji 65, huku, straika wa Fountain Gate, Selemani Mwalimu akiwa kinara, akipachika magoli matano mpaka sasa.

Takwimu zinaonyesha kati ya mabao hayo, 10 yamefungwa kwa penalti na moja la kujifunga.

Waliofunga mabao kwa penalti ni Djuma Shaaban wa Namungo, Heritier Makambo na Shedrack Asiegbu (Tabora United), Jean Ahoua na Leonel Ateba (Simba), Ibrahim Elias (KMC), Salum Kihimbwa (Fountaina Gate), Hassan Dilunga (JKT Tanzania), Nurdin Chona (Prisons) na Stephane Aziz Ki wa Yanga.

Fred Tangalo wa KMC, alijifunga katika harakati za kuokoa katika mchezo ulichezwa Septemba 19, mwaka huu wakati timu yake ikipata kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Azam FC, likiwa ni bao pekee la kujifunga tangu kuanza kwa msimu huu.

Katika mabao hayo 91, Fountain Gate ndiyo iliyofunga mengi zaidi mpaka sasa, ikipachika mabao 14, ikifuatiwa na Simba yenye mabao 12, huku Pamba Jiji ikifunga mabao mawili tu ambayo ni machache zaidi kufungwa na timu kwenye ligi mpaka sasa.

Takwimu zinaonyesha katika michezo 50 ya Ligi Kuu iliyochezwa mpaka sasa, 33 imetoa washindi na 17 imemalizika kwa sare.

Pia katika michezo 33 ya ushindi, mechi 19 timu zimeshinda zikicheza viwanja vya nyumbani, na michezo 14 imetoa washindi timu zikicheza ugenini.

Ratiba inaonyesha Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea tena Oktoba 18, mwaka huu ambapo michezo ya raundi ya nane itaanza, Coastal Union itaikaribisha Dodoma Jiji, JKT Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tabora United na Prisons itakuwa nyumbani dhidi ya Azam FC.

Oktoba 19, kutakuwa na patashika nguo kuchanika miamba miwili ya soka nchini, Simba ya Yanga zitavaana, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku Oktoba 20, Singida Black Stars itacheza dhidi ya Namungo na Fountain Gate itawaalika KMC.




Wachezaji chipukizi wa wavu ya ufukweni wa umri kati ya miaka 15 na 20, wakiwa katika mafunzo maalumu ya mchezo huo yaliyofanyika wiki iliyopita Visiwani Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

# Mtibwa, Songea United hapatoshi

Na Somoe Ng'itu

LIGI ya Championship inatarajia kuendelea tena kesho kwa vinara Mtibwa Sugar kuwakaribisha Songea United kutoka Ruvuma katika mchezo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Manungu ulioko Turiani mkoani, Morogoro.

Mtibwa Sugar yenye pointi tisa sawa na Songea United na Stand United ya Shinyanga ndio vinara katika msimamo wa Ligi ya Championship.

Mkuu wa msafara wa Songea United, James Mhagama, aliliambia gazeti hili kikosi chake kiliweka kambi mkoani hapo na kinaendelea vyema na maandalizi kwa ajili ya mechi hiyo.

Mhagama alisema wachezaji wao wako tayari kupambana na Mtibwa Sugar na wamejiandaa kukutana na mchezo wenye ushindani kwa sababu wanafahamu wapinzani wao wanauzoefu zaidi.

"Tuko hapa (Morogoro), tunaendelea na maandalizi, tutawafuata Mtibwa kule Manungu na huko tunaenda na jambo moja tu la kusaka pointi tatu muhimu, tunajua haitakuwa rahisi kwa kila upande," alisema Mhagama.

Aliongeza malengo ya timu yao ni kupambana na kuhakikisha wanapanda daraja katika msimu ujao ili kuwapa furaha mashabiki wao wa Ruvuma.

Kiluvya ya Pwani na Transit Camp ambazo hazina pointi hata moja zinaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo.

## Taifa Stars, DR Congo

INATOKA UK. 24

wazi hisia zao na mapenzi kwa mchezaji huyo wa zamani wa mabingwa wa Afrika, TP Mazembe yenye makazi yake Lubumbashi.

"Kwenye kikosi cha Tanzania tunamhofia zaidi Samatta, ni mchezaji mzuri na amefanya makubwa hapa akiwa na TP Mazembe, wengi tutakwenda uwanjani kumwangalia, lakini tunataka Congo ishinde," alisema mmoja wa mashabiki ambaye ni Mkongomani.

Samatta alicheza kwa mafanikio makubwa akiwa na TP Mazembe aliyojiunga nayo mwaka 2011 akitokea Simba na alifikia kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani.

## Simba, Yanga zafunguka

INATOKA UK. 24

Yanga kimeanza rasmi mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa dabi huku wakiahidi wataendeleza vipigo kama kawaida.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, aliliambia gazeti hili baada ya mapumziko ya muda mfupi, wachezaji wa timu hiyo ambao hawakuitwa kwenye vikosi vya timu za taifa walirejea mazoezini ili kujiandaa na mchezo huo muhimu.

"Tulikuwa na mapumziko mafupi, lakini tumerejea tena na hii ni kwa ajili ya wachezaji ambao hawakupata nafasi ya kuziwakilisha nchi zao katika michezo ya kimataifa, kila kitu kinaenda vizuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Simba. Wachezaji waliobaki wanajiandaa vyema ili wenzao wakirejea wote wawe na utimamu wa mwili, programu hii itawapa wanachama na mashabiki wa Yanga kile ambacho tunakitarajia," alisema meneja huyo.

Aliwataka mashabiki wa Yanga wasiwe na wasiwasi kwa sababu kikosi chao kipo imara na wana matumaini ya kuendelea kuwapa furaha kwa kuendeleza kilio kwa wapinzani wao.

"Hatujawaambia wachezaji wetu wajilinde wakiwa kwenye timu za taifa ili wasiumie wasije kukosa mchezo dhidi ya Simba, hapana, tunataka wapambane kwenye timu zao kwa sababu wakifanya hivyo pia ni sifa kwa Yanga, na inaongeza wigo wa kutoa wachezaji wengi zaidi siku za mbele, sisi tunaamini watarejea salama salmini na kuwahi kucheza mechi hiyo na nyingine bila ya kupata majeraha," aliongeza meneja huyo.

Yanga kwa siku za karibuni imekuwa mbabe kwa Simba, ikishinda michezo mitatu mfululizo, miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara na mmoja wa hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii.

Mara ya mwisho kukutana ilikuwa ni Agosti 8, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikishinda bao 1-0.

Michezo

Nipa...

Alhamisi Oktoba 10, 2024

**Messi, Madrid wafunguka Iniesta akistaafu kimataifa**

UKURASA 22





Kiungo wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Hijjah Lidah (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Djibouti, Mohamed Omar katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya CECAFA U-20 iliyofanyika kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Ngorongoro Heroes ilishinda mabao 7-0.
**PICHA: TFF**

# STARS, DR CONGO MAJARIBUNI LEO

## ●●●Samatta ateka mapokezi Kinshasa, Morocco atamba anataka...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI ikiwa ugenini kusaka pointi tatu muhimu, Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Suleiman 'Morocco', amesema malengo yao ni kuona wanaongoza katika Kundi H na hatimaye kufikia malengo ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), zitakazofanyika baadaye mwakani nchini Morocco.

Hata hivyo, wakati Stars inatua mjini Kinshasa, mshambuliaji nyota wa timu hiyo, Mbwana Samatta, aligeuka kivutio kwa mashabiki waliojitokeza na hiyo inaonyesha heshima kwa Mtanzania huyo aliyewahi kuichezea TP Mazembe ya nchini humo.

Timu hizo zinakutana huku wenyeji wenye pointi sita wakiwa kinara katika Kundi H wakifuatiwa na Taifa Stars iliyojikusanyia pointi nne, Ethiopia yenye pointi moja inashika nafasi ya tatu huku Guinea wakiburuza mkia kutokana na kutokuwa na pointi yoyote.

Akizungumza na gazeti hili kuelekea mechi hiyo, Morocco, alisema anaiheshimu DRC Congo lakini malengo yake ni kupata ushindi katika mchezo wa leo ili kujiweka kileleni kwenye msimamo wa kundi.

"Nafahamu hautakuwa mchezo mwepesi, tupo ugenini, lakini lazima tupambane kufikia malengo yetu, ni mchezo ambao ushindi utatuweka juu katika msimamo wa kundi. Tumejiandaa vizuri lakini tutacheza kwa nidhamu kubwa kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kuondoka na pointi tatu," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema akili na nguvu zao zote wamezielekeza katika mchezo huo utakaoanza saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

"Baada ya mchezo ndio sasa tutaanza kuupigia mahesabu mchezo wa marudiano ambao tutakuwa nyumbani, nina imani na kikosi changu na kila mchezaji yupo kwenye morali na ari nzuri," Morocco alisema.

Naye nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema wako tayari na ushirikiano 'mkubwa' waliopata kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, umewaongezea chachu ya kwenda kupambana.

Alisema wanaona wanadeni la kuwalipa Watanzania na njia pekee ni kupambana na kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo.

"Kikubwa cha kuwalipa Watanzania ni kufanya vizuri," alisema beki huyo anayeichezea Simba ya Dar es Salaam.

Katika hali iliyoamsha shangwe, Samatta, ambaye amerejeshwa katika kikosi cha timu hiyo baada ya kuwa nje kwenye mechi mbili zilizopita, amekuwa gumzo Congo ambapo mashabiki wengi wanamzungumzia.

Wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege Mjini Kinshasa, mashabiki hao waliweka

INAENDELEA UK. 23

# Simba, Yanga zafunguka

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema malengo yake ni kumaliza kinara katika Kundi A kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika watani zao, Yanga wanawaza kutoa kichapo katika mechi ya dabi itakayochezwa Oktoba 19, mwaka huu.

Simba imepangwa Kundi A pamoja na CS Costantine ya Algeria, CS Sfaxien kutoka Tunisia na Bravo do Maquis ya Angola.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Fadlu alisema baada ya ratiba hiyo kutoka, ameanza kuandaa mikakati ya kuhakikisha wanafuzu hatua inayofuata mapema zaidi na kuwa kinara kwenye kundi hilo.

Fadlu alisema anajua kundi hilo ni gumu na haitakuwa rahisi kutimiza malengo yake badala yake kazi ya ziada inatakiwa kufanyika.

"Makundi nimeyaona, timu za kundi letu pia nimeziona, pamoja na hayo mipango yetu ni kufuzu mapema zaidi na kuwa vinara ya kundi hili, hatua ya makundi unatakiwa kushinda mechi zako nyumbani, lakini haiwezekani ukafanya hivyo kirahisi kama hujaandaa kikosi, pia mikakati mingi ya kimbinu na kiufundi kuhakikisha unashinda.

Ukweli unabaki pale pale kundi gumu, siku zote ukipangiwa na timu za Afrika Kaskazini ujue umekutana na ugumu, CS Costantine na CS Sfaxien ni timu za Kaskazini, na hili tumeliona wakati tulipocheza dhidi ya Al Ahli Tripoli, lakini nadhani mchezo ule umetupa uzoefu kwa wachezaji ambao walikuwa hawajawahi kukutana na timu za aina ile na mashabiki wake, hivyo watakuwa wameshaanza kuzizoea," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema wakati wanaendelea na maandalizi ya kuwakabili Yanga, pia wanajipanga na mechi za hatua ya makundi ambapo Novemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam watakaribisha Bravo do Maquis kutoka Angola.

"Haya ni maandaalizi ya jumla, tutacheza dhidi ya Yanga, Oktoba 18, mwaka huu lakini hapo hapo tutakuwa tunaelekea katika mechi ya kimataifa, tutaanza nyumbani na itabidi tushinde ili tuanze kujiamini kuelekea kuongoza kundi letu," Fadlu alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >